UMWAFAKA WA FASIHI YA WATOTO KWA MISINGI YA MWITIKIO WA MTOTO MSOMAJI: MFANO WA VITABU VITATU VILIVYOANDIKWA NA KEN WALIBORA.

NA

KYEU D. WAMBUA

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Eger233903

2009/78870

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutosholeza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili (Kiswahili) katika idara ya fasihi, lugha na isimu chuo kikuu cha Egerton

EGERTON UNIVERSITY 2008.

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote kile.

Sahihi..... Tarehe.12/07/08.....

Kyeu, D. Wambua.

AM12/1141/04

IDHINI

Tasnifu hii ya shahada ya Uzamili imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi wa mtahiniwa katika chuo kikuu cha Egerton.

Sahihi..... Tarehe.18.7.2008

Dkt. Onyango, J. Ogola.

HATILINZI
©2008
DAVID WAMBUA KYEU
Haki za kunakili kwa njia yoyote ile ni ya mwandishi na chuo kikuu cha Egerton.

KUTABARUKU

Kwa wazazi wangu Bw. Solomon Kyeu mwanaa Wambua na Christine Kingi wa Kyeu: Kazi hii ni shukrani kwenu kwa mengi mliyojihini kwa ajili yangu.

Kwa mke wangu Nancy Wanjiru wa Wambua: Mwenyezi akubariki kwa uvumilivu wako katika kipindi kizima cha utafiti.

Kwa ndugu zangu marehemu Esther Kisaya, kaka Joshua Valua na Peter Makau: Ufanisi wa kazi hii umekidhi sala zenu za tangu utotoni.

Kwa mpwa wangu mpendwa Tito Muimi: Usomi alionijalia MAULANA uwe dira kwako japo si lazima uegemee Lugha ya Kiswahili.

SHUKRANI

Kazi hii ingekuwa ndoto tu endapo Mwenyezi Mungu hangenijalia katika kipindi chote cha utafiti. Mwenyezi Mungu alinisaidia kushirikiana na wataalamu kadha wa kadha ambao michango yao ilinoa fikra zangu kabla ya kuchukua kalamu na kuandika tasnifu hii. Huenda nisitaje baadhi yao maanake idadi ni kubwa mno. Hivyo basi naomba wasiotajwa waniwie radhi maanake sikufanya hivyo kwa hiari. Nawashukuruni nyote mliochangia kwa njia moja au nyingine katika kuukamilisha utafiti huu.

Shukrani jazila ni kwa msimamizi na mwelekezi wangu Dkt. James Ogola Onyango. Alinielekeza tangu mradi huu ulipokuwa wazo tu hadi hivi leo mradi umezaa tasnifu. Namshukuru kwa jinsi ambavyo aliniongoza katika majadiliano ya ana kwa ana na pia katika kuzisoma makala mbalimbali nilizompa, akazihakiki kisha akatenga wakati wake adimu ili kujadiliana naye na kunikosoa.

Shukrani jazila zimwendee mwenyekiti wa idara ya Lugha na Isimu Dkt. Catherine Kitetu ambaye alinikumbusha kila mara kwamba nilikuwa na wajibu wa kukamilisha mradi huu. Katika kitengo hiki, vilevile, nawashukuru wahadhiri Dkt. Mwenda Mukuthuria, Wendo Nabea,, Dkt. Merle Krueger na Prof. Magdalena Hauner ambao walichonga fikra zangu na kuziweka katika mkondo wa kiakademia. Madaktari Beja Karisa na Furaha Tchai walinitumbukiza vyema katika bahari ya Kiswahili na kunifunza kuogelea.

Mke wangu Nancy Wanjiru namshukuru sana kwa kunivumilia wakati huu wa usomi. Hiki kilikuwa kipindi cha majaribu, hata hivyo alinitia moyo na kunipa nafasi ya kuwekeza kwa hali na mali katika tasnifu hii. Hewala majaaliwa ya Mwenyezi Mungu utashuhudia matunda ya uwekezaji kama huu.

Nawashukuru pia ndugu zangu Joshua Valua na Peter Makau kwa kunipa moyo katika kipndi kizima cha utafiti. Waliyafidia majukumu yangu kwa hali na mali wakati ambao sikuwapo. Mpwa wangu Titus Muimi alichangia pakubwa pia katika utafiti huu. Yeye mwenyewe ndiye aliyetumbukiza mkono katika kapu na kuniteulia shule mbili ambazo zilishirikishwa katika utafiti.

Shukrani za dhati pia ziwaendee wasomi wenzangu wa Kiswahili. Gacheiya Mwaura alitenga wakati wake kila mara kujadiliana nami kuhusu utafiti wangu. Wengine ni Riro Matinde, Ojwang' Steve (Mwiba tosha), akina Stanley na Alex Kevogo, Minyori Mureithi (Daddy). Hawa kwa kweli walijenga mazingira mufti ya kukua kwa wazo langu hadi pale lilikuwa tasnifu. Ndani mwao nilipata visawe sugu vya Kiswahili kando na kunifaidi kwa mijadala tuliyokuwa nayo mara kwa mara.

Litakuwa kosa la jinai endapo sitowashukuru wakutubi na wafanyakazi wa maktaba za vyuo vikuu vya Egerton, Kenyatta, Nairobi, Brown na Wisconsin. Hawa waliniruhusu kupitia baadhi ya vitabu vyao. Waliniruhusu nyakati zingine kuzipitia malighafi zao licha ya kuwa na upungufu wa pesa za kulipa ada ya kuingia maktabani. Wizara ya Elimu nayo mjini Thika ilinipa idadi ya shule zilizokuwa Wilayani. Idara ya elimu vilevile ilinielekeza kutambua kunakopatikana shule mbili zilizoshirikishwa katika utafiti.

Walimu wa shule za msingi za Nyamang'ara na Athena pia sitoahini shukrani zangu. Walinikaribisha kwa mikono miwili kando na kunisaidia kuteua sampuli ya wanafunzi walioshirikishwa katika utafiti. Wanafunzi wote 60 walioshiriki katika utafiti huu pia nawashukuru sana. Haingekuwa wao basi hamngekuwa deta ya kuchanganuliwa.

IKISIRI

Utafiti huu ulijikita kuchunguza umwafaka wa fasihi ya watoto iliyoandikwa na Ken Walibora kwa misingi ya Mwitikio wa mtoto msomaji. Vitabu nilivyovirejelea vilikuwa, *Mtu wa Mvua, Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni*. Utafiti huu ulichochewa na maoni kutoka kwa wataalamu mbalimbali kwamba ipo haja kubwa ya kufanyia utafiti mwitikio wa mtoto msomaji anapoisoma kazi yoyote ya fasihi. Hii ni kwa sababu, sio lazima alichoandikiwa mtoto na msanii aliyekomaa kiumri kiwe cha kumridhisha. Utafiti huu ulithibitiwa na chukulizi zifuatazo; (1) Kwamba fasihi ya mtoto inastahili kumjuza mtoto maswala muhimu huku ikimridhisha kutokana na umbile lake. (2) Kitabu kizuri cha fasihi ya watoto ni kile ambacho yaliyomo na umbile jumla la kitabu yamesanwa kwa muumano ulio mzuri machoni pa mtoto msomaji. (3) Mchunguzi mufti wa fasihi ya watoto ni mtoto mwenyewe. (4) Uchunguzi endelevu wa fasihi hii unapelekea uzalishwaji bora wa fasihi hii. Ili kufanikisha utafiti huu, niliongozwa na Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Nadharia hii ilinisaidia kuchunguza kwa undani mwitikio wa watoto wasomaji kwa vipengele mbalimbali vilivyoviumba vitabu nilivyovirejelea. Utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani. Uteuzi sampuli wa mtabakisho na uteuzi sahili kishelabela ulitumika ili kuhakikisha kwamba watoto wa aina mbalimbali wameshirikishwa. Wanafunzi wa darasa la 7 na 8 walio kati ya umri wa miaka 12 na 16 waliteuliwa kutoka shule mbili za msingi wilayani Thika. Njia za kukusanya deta zilizotumika zilikuwa uchunguzi shiriki, hojaji na mahojiano. Deta ilichanganuliwa kwa kuzingatia umaratokezi wa majibu. Majedwali yalitumika kurahisisha uchanganuzi , huku asilimia zikitumika kupima uzito wa majibu yaliyopatikana. Grafu kwapao ilitumika mwishoni kuonyesha miitikio ya kijumla kutokana na hatua zote za utafiti na vilevile

kubainisha kazi iliyokuwa mwafaka zaidi kwa mtoto msomaji. Matokeo ya utafiti huu yaliweka bayana kwamba watoto wasomaji walikuwa na miitikio kwa vipengele mbalimbali vinavyojenga vitabu vya fasihi ya watoto vilivyotumika. Aidha, kwa misingi hiyo basi waliweza kujiteulia wao wenyewe kitabu mwafaka ambacho kilikuwa *Mtu wa Mvua*, kilichowaridhisha zaidi ya *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni*. Utafiti huu unatarajiwa kuwa muhimu sana kwa wahusika mbalimbali wa fasihi ya watoto. Miongoni mwa hawa ni wapangaji sera za elimu ya watoto, wahakiki wa fasihi ya watoto, wataalamu, waandishi na wachapishaji wa faishi ya watoto, waratibu mitaala ya fasihi ya watoto, waandishi na mashirika ya uchapishaji wa fasihi ya watoto, wazalishaji wa fasihi ya watoto katika vyombo vya habari, maktaba na wataalamu wa fasihi ya watoto katika vyuo vikuu.

ABSTRACT

The purpose of this research was to find out the appropriateness of Swahili children's literature written by Ken Walibora on the basis of child-reader responses. The reference texts used were *Mtu wa Mvua*, *Ndoto ya Amerika* and *Mgomba Changaraweni*. The research was in consonance with many suggestions by children's literature scholars that there was need for research on reader-responses because having children literature written by adults was no guarantee that readers would follow. Underlying the study were four theoretical assumptions. (1) Was that children's literature should communicate important values to the child as well as benefit him/her aesthetically. (2) Was that the best children's book was the one which form and content operated in harmony. (3) Thirdly was that the best critic of children's book was the child him/herself. (4) Was that critical works enhanced quality of Children's literature. The theoretical framework of the research was Reader-Response Theory advanced by Fish (1981) and Rosenblatt (1938). This theory tries to find out how readers respond to the literary elements as they go through a work of art. The research adopted fieldwork design. Observations, questionnaires and interviews were the methodologies used to collect data. The target population was Standard 7 and 8 pupils of Thika District Primary Schools whose age ranged between 12- 16 years. Stratified and simple random sampling techniques were used to select a representative sample of the target population. Data collected were analyzed using descriptive statistics. Tables, percentages and a bar graph/s were used to simplify data obtained. Upon completion, the research revealed that children readers had responses to various literary aspects of literature written for them. The child reader also went further to select the most appropriate book. The findings revealed that children

found the book *Mtu wa Mvua* more appropriate for them than the other two texts. This research is meant to be of immense importance to various stakeholders. Amongst them being literary critics, children's literature specilalists, writers and publishers. Libraries and media houses and chidren literature curriculum developers are also meant to benefit from these findings.

YALIYOMO

UNGAMO.....i

HATILINZI.....ii

KUTABARUKU.....iii

SHUKRANI.....iv

IKISIRI.....vi

ABSTRACT.....viii

YALIYOMO.....x

DIBAJI YA MAJEDWALI NA GRAFU KWAPAO.....xiii

MAELEZO YA ISTILAHI.....xiv

SURA YA KWANZA.....1

1.0 UJENZI WA UTAFITI.....1

1.1 Utangulizi.....1

1.2 Usuli wa mada.....2

1.3 Mada ya utafiti.....3

1.4 Madhumuni ya utafiti.....3

1.5 Nadharia tete za utafiti.....3

1.6 Umuhimu wa utafiti huu.....4

1.7 Upeo na mipaka ya tasnifu.....6

SURA YA PILI.....7

2.0YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI.....7

2.1Utangulizi.....7

2.2Historia ya fasihi ya watoto.....8

2.2.1 Enzi ya kale ya Kirumi (50 BCE-500 BCE).....8

2.2.2 Enzi ya kati (500-1500 CE).....9

2.2.3 Enzi ya kuchipuka upya kwa bara Ulaya (1500-1650).....9

2.2.4 Karne ya 17.....10

2.2.5 Karne ya 18 na 19.....12

2.2.6 Enzi ya Malkia Victoria.....13

2.2.7 Karne ya 20 :kutanuka kwa ulimwengu.....14
2.3 Fasihi ya watoto nchini Kenya..... 15
2.4 Dhima ya fasihi ya mtoto.....19
2.5 Mapitio zaidi ya maandishi- Tasnifu.....19
2.6 Mwandishi Ken Walibora.....27
2.7 Msingi wa nadharia.....28
2.7.1 Nadharia ya Mwitikio wa msomaji.....29
2.7.2 Misingi ya nadharia hii.....31
2.8 Muhutasari wa vitabu.....33
2.8.1 Mtu wa Mvua.....33
2.8.1.1 Sungura Hasara.....33
2.8.1.2 Mtu wa Mvua.....34
2.8.1.3 Charo na Watoto Watoro.....35
2.8.2 Ndoto ya Amerika.....36
2.8.3 Mgomba Changaraweni.....37
2.9 Hitimisho.....37

SURA YA TATU.....39
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....39
3.1 Utangulizi.....39
3.2 Utaratibu wa utafiti.....39
3.3 Uteuzi wa sampuli.....40
3.4 Mbinu za ukusanyaji deta.....40
3.5 Vifaa vya utafiti.....40
3.6 Uchanganuzi wa deta.....41

SURA YA NNE.....43
4.0 UCHANGANUZI WA MIITIKIO.....43
4.1 Utangulizi.....43
4.2 Miitikio ya mtoto msomaji katika hatua ya kwanza.....43
4.3 Uchanganuzi wa miitikio iliyokusanywa kwa kutumia hojaji.....48

4.3.1Maudhui/ Mafunzo.....48
4.3.2 Anwani ya vitabu.....50
4.3.3 Majalada ya vitabu.....51
4.3.4 Wahusika.....52
4.3.5 Ugumu/Wepesi wa hadithi.....54
4.3.6 Matumizi ya picha.....56
4.3.7 Lugha katika vitabu vyote vitatu.....58
4.3.8 Umwafaka wa vitabu.....59
4.3.9 Idadi ya hadithi katika kitabu.....60
4.4 Hitimisho.....61

SURA YA TANO.....63
5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....63
5.1 Utangulizi.....63
5.2 Hitimisho.....63
5.3 Mapendekezo.....64
MAREJELEO.....66
VIAMBATISHO.....72
Kiambatisho A (Hojaji).....72
Kiambatisho B (Maswali ya mahojiano).....77

DIBAJI YA MAJEDWALI NA GRAFU KWAPAO

1. Jedwali 1. Miitikio katika hatua ya kwanza ya uteuzi wa vitabu.....44
2. Jedwali 2. Asilimia katika uteuzi wa vitabu.....48
3. Jedwali 3. Asilimia za swali la maudhui/ Mafunzo.....49
4. Jedwali 4. Swali la anwani ya vitabu.....50
5. Jedwali 5. Majalada ya vitabu.....51
6. Jedwali 6.Wahusika.....52
7. Jedwali 7. Ugumu/Wepesi wa hadithi.....54
8. Jedwali 8.Matumizi ya picha.....57
9. Jedwali 9.Lugha katika vitabu vyote vitatu.....58
10. Jedwali 10.Umwafaka wa vitabu.....59
11. Jedwali 11.Idadi ya hadithi katika vitabu.....60
12. Jedwali 12.Wastani jumla wa miitikio kutokana na hojaji.....61
13. Grafu ya 1.Grafu kwapao ya umwafaka wa vitabu.....62

MAELEZO YA ISTILLAHI

1. Umwafaka

Neno hili lilipotumika katika utafiti huu lilimaanisha ukubalifu. Kwa mfano; Ukubalifu wa fasihi ya watoto. http://dictionary.cambridge.org/define.asp?key=3672&dict=CALD

2. Mwitikio wa msomaji.

Ni jinsi ambavyo msomaji wa kazi fulani iliyoandikwa huipokea na kuathiriwa nayo. Kuathiriwa kwake hutambulika kutokana na Maoni anayotoa kuihusu au hulka anazozielekeza kwa kazi yenyewe.

http://www.yourdictionary.com/ahd/r/r0182400.html

3. Uteuzi wa sampuli wa mtabakisho.

Hapa, jumuiya iliwekwa katika makundi kwanza kabla ya uteuzi sampuli kufanywa. Makundi yaliyoteuliwa kama sampuli ya utafiti yalikuwa kwa misingi ya kijinsia.

http://dictionary.cambridge.org/define.asp?key=78683&dict=CALD

4. Kipimo cha Likert.

Ni mfumo unaotumika kupima dhana zenye viashiria vingi. Mhojiwa alipewa maswali aliyohitaji kutoa maoni. Aghalabu majibu waliyotoa wahojiwa yalionyesha kiwango cha kukubaliana.

http://encyclopedia.thefreedictionary.com/Likert+scale

5. Uteuzi sahihi wa Kishelabela.

Mbinu hii ya uteuzi uhakikisha kwamba kila mtu ana uwezo sawa wa kuteuliwa na kuwekwa katika kundi la sampuli kutoka kwa jumuiya lengwa. Nilifanya hivi kwa kuandika vikaratasi vya majina yote ya jumuiya. Baadaye nilichanganya vikaratasi hivyo kisha nikateua vikaratasi 2 vya shule nilivyohitaji katika utafiti.

http://en.wikipedia.org/wiki/Sampling_(statistics)

6. Watoto wa aina mbalimbali.

Ilipotumika ilimaanisha sampuli ya watoto kusawazishwa katika misingi ya kijinsia, tajriba, na maeneo ya kuishi (mjni au vijijini.)

7. BCE

Ilipotumika ilimaanisha kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

SURA YA KWANZA

1.0 UJENZI WA UTAFITI

1.1 Utangulizi.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza inatanguliza mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete za utafiti na upeo wa utafiti. Sura ya pili inagusia mapitio ya maandishi mbalimbali. Katika sura hii, maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu fasihi ya watoto yamefafanuliwa. Maoni mengi yaliyofafanuliwa hasa ni yale yaliyohusiana na mwitikio wa mtoto msomaji kwa fasihi ya watoto. Hata hivyo, maoni mengine ya kijumla kuhusu fasihi ya watoto yalifafanuliwa pia. Katika sura hii pia, maelezo kuhusu historia ya maendeleo ya fasihi ya watoto pamoja na maelezo kumhusu mwandishi Ken Walibora ambaye vitabu vyake vilitumika katika utafiti yalipatikana. Kwa kupitia maandishi mbalimbali na historia ya mtoto, upungufu wa kutokuwepo ushirikishi wa mtoto msomaji uliwekwa wazi. Aidha ufafanuzi wa msingi wa nadharia iliyotumika ulipatikana katika sura hii vilevile. Sura ya tatu nayo ilishughulikia mbinu za utafiti zilizotumika. Katika sura ya nne, ndipo tunapata uchanganuzi wa miitikio mbalimbali iliyopatikana. Deta ilichanganuliwa kutegemea madhumuni ya utafiti na kuwekwa kimuhutasari kwa kutumia majedwali. Tasnifu hii ilikamilishwa kwa maelezo ya sura ya tano. Muhutasari, hitimisho na mapendekezo yalitolewa katika sura hii.

1.2 Usuli wa mada

Hatua zote za uzalishaji wa fasihi ya watoto hazimchukulii mtoto kuwa mhusika muhimu licha kwamba yeye ndiye hadhira lengwa. Ni dhahiri kwamba hali hii imepelekea kupotoshwa kwa wahusika mbalimbali wakiwemo wazazi, wapangaji sera za elimu na walimu kuhusu fasihi inayostahili kupendekezwa kwa watoto. Nyambura (1995) anasema kwamba haiwezekani mhakiki aliyekomaa kumtendea haki mtoto anapomchunguzia fasihi inayomlenga. Hali hii inaungwa mkono na Hunt (1992:162) anaposema kwamba:

> "Maswala yanayoweza kuonekana muhimu machoni pa mhakiki aliyekomaakiumri kuhusu kitabu fulani cha fasihi ya watoto hienda yakakosa mantiki kwa mtoto msomaji. (tafsiri hii na nyingine zitakazofuata ni zangu)

Garner akinukuliwa na Hunt (1992:163) anaunga mkono kauli hii. Kwamba huenda mzazi akamnunulia mwanawe kitabu cha fasihi kutokana na maadili yaliyokita kwacho, hatimaye akagundua kwamba kitabu hiki hakimridhishi kamwe.

Mwitikio wa mtoto msomaji kwa fasihi aliyoandikiwa katika lugha ya Kiswahili umepuuzwa kwa muda mrefu huku watu wakitegemea na kuamini maoni na tahakiki za wachunguzi/wahakiki waliokomaa kiumri. Nyambura (1995) na Hunt (1992) wanasema kwamba, mhakiki anayefaa wa kazi yoyote ile ni hadhira lengwa. Hawa wanasisitiza kwamba hamna haja ya mhakiki aliyekomaa kiumri kujitoma katika kazi ya mtoto maanake mtoto mwenyewe anatosha. Kwamba mtoto anao uwezo wa kuibua miitikio mbambali kwa vipengele mbalimbali vilivyotumiwa. Utafiti huu utatumia mwitikio wa

mtoto msomaji kuzichunguza kazi alizowaandikia watoto mwandishi Ken Walibora. Utafiti huu uliweka bayana miitikio ya watoto wasomaji na kupendekeza iwapo ni chombo mufti cha kutathmini fasihi ya watoto iliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili.

1.3 Mada ya Utafiti.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza umwafaka wa fasihi ya watoto iliyoandikwa na Ken Walibora kwa misingi ya mwitiko wa mtoto msomaji katika vitabu vitatu vya *Mtu wa Mvua, Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni.*

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo;

(i) Kuchunguza miitikio ya mtoto msomaji anapochagua na kusoma kitabu miongoni mwa vitabu vya fasihi ya watoto.

(ii) Kubainisha umwafaka wa vitabu hivi kwa misingi ya miitikio ya watoto wasomaji.

1.5 Nadharia tete za utafiti

1. Miitikio mbambali huzuka mtoto anapoteua na kusoma kitabu miongoni mwa vitatu vilivyoandikwa na Ken Walibora.
2. Vitabu hivi vina mwafaka tofauti katika misingi ya mwitikio wa mtoto msomaji.

1.6 Umuhimu wa utafiti huu

Utafiti huu unatarajiwa kuwa muhimu kwa wahakiki wa fasihi ya mtoto. Kwa muda mrefu maoni ya wahakiki waliokomaa yamekuwa yakiaminiwa sana katika shughuli za kumteulia mtoto fasihi ya kusoma. Utafiti huu unapendekeza kwamba maoni ya mtoto yanastahili kushirikishwa pia kutegemea namna ambavyo anaitikia kazi aliyoandikiwa.

Utafiti huu ulitarajiwa kuwa kurunzi kwa wapangaji sera za elimu ya mtoto na waratibu mitaala. Uchunguzi uliofanywa na watu waliokomaa umekuwa ukitegemewa kwa muda mrefu kupendekeza kazi za fasihi ya watoto kwa mtoto. Utafiti ambao ulifanywa na Nyambura (1995) ulionyesha kuwa mtoto msomaji anaitikia fasihi ya watoto kwa njia mbalimbali. Miitikio hii imetumiwa mwishoni mwa utafiti kubainisha kitabu kilicho mwafaka zaidi kwa mtoto msomaji. Matokeo haya yanatarajiwa kuwaelekeza wataalamu kubuni mikakati kuhakikisha kwamba mtoto ameshirikishwa katika kuteua fasihi inayomlenga kabla ya kupitishwa kuwa fasihi mwafaka na wahakiki waliokomaa kiumri.

Waandishi na wachapishaji wengi wamejifunga kibwebwe kuzalisha vitabu bila kujali maslahi ya watoto. Hapa nikimaanisha kwamba licha ya fasihi kumpa mtoto maadili ya jamii, inastahili kumridhisha kutokana na umbile lake kijumla. Utafiti uliofanywa umedhihirisha kwamba mtoto huvutiwa na vipengele mbalimbali vya kitabu alichoandikiwa na mwandishi mkomavu. Aidha imedhihirika wazi kwamba watoto wana hamu ya kitabu kinachowaburudisha licha ya kuwapa mafunzo. Hivyo basi, uchunguzi wa sampuli hii utawasaidia waandishi na wachapishaji katika kuchunguza miswada mbalimbali kwa misingi ya mwitikio wa mtoto msomaji kabla ya kuichapisha.

Kwa upande mwingine, wazazi wamekuwa wakiwanunulia watoto vitabu kwa sababu vina anwani nzuri iliyosheheni maadili. Aidha, wao hufanya hivi pasipo kutilia maanani umbile la kitabu chenyewe na maudhui yaliyokita katika kitabu. Nyakati zingine wao huwanunulia wana wao vitabu hivi kutokana na maoni ya wahakiki waliokomaa kwamba kitabu fulani ni kizuri kwa mtoto. Utafiti uliofanywa umedhihirisha kwamba anwani ya kitabu si kipengele pweke muhimu machoni pa mtoto msomaji. Hivyo basi, utafiti huu utawaangazia wazazi vipengele muhimu vya kuzingatia kabla ya kuwanunulia wana wao kitabu chochote cha fasihi.

Sekta ya uzalishaji vipindi vya runinga na redio kwa watoto inatarajiwa kunufaika na utafiti huu kwa sababu watawazalishia watoto vipindi ambavyo wamevipenda. Utafiti huu vilevile utafaidi maktaba mbalimbali zilizo na vitengo vya fasihi ya watoto. Aidha wakutubi sasa watawekeza mitaji yao katika vitabu ambavyo vinapendeka na watoto.

Mwishowe utafiti huu unatarajiwa kuwa changamoto kwa wataalamu wa fasihi ya watoto katika vyuo vikuu. Kwamba hakujakuwepo mfumo mufti wa kufunza fasihi ya watoto iliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili kutokana na kasumba kwamba fasihi hii ni kitengo cha fasihi pana inayojumlisha fasihi ya hadhira komavu. Hivyo,basi ikawa utafiti wake unawekwa pamoja na ule wa hadhira komavu (Hunt 1992). Utafiti huu utakuwa hamasisho kwamba fasihi ya watoto ni kitengo maalum kinachohitaji kufunzwa na kuwekewa mikakati maalum kama taaluma nyingine yoyote ile. Wataalamu watakaozaliwa ndio watakuwa chemichemi na walezi wa utanzu huu, wauchunge ili usife au kutiwa najisi na washikadau walaghai.

1.7 Upeo na mipaka ya tasnifu.

Kuna wadau wengi wanaoweza kutoa maoni yao kuhusiana na fasihi ya watoto. Hunt (1992) anasema baadhi ya hawa wanaweza kuwa wazazi, vyombo vya habari, watoto, wahakiki waliokomaa kiumri na waandishi wenyewe. Katika utafiti huu, nilizingatia mwitikio wa mtoto msomaji pekee. Utafiti huu ulichunguza;

(a) Miitikio ya mtoto msomaji kwa wahusika.

(b) Miitikio ya mtoto msomaji kwa kiwango cha lugha alichozingatia mwandishi.

(c) Miitikio ya mtoto msomaji kwa hati zilizotumika.

(d) Miitikio ya mtoto msomaji kwa picha alizozitumia mwandishi.

(e) Miitikio ya mtoto msomaji kwa anwani ya kitabu.

(f) Miitikio ya mtoto msomaji kwa umbile la jalada la kitabu

(g) Miitikio ya mtoto msomaji kwa maudhui aliyoshughulikia mwandishi.

Watoto walioshirikishwa katika utafiti huu walikuwa wa darasa la 7na 8 pekee waliokuwa na umri kati ya miaka 12 na 16 na waliofanya vyema katika soma la Kiswahili. Umri wa chini zaidi wa mtoto katika sampuli iliyoteuliwa ulikuwa wa miaka 12 kisha wa juu zaidi ulikuwa wa miaka 16. Utafiti huu ulishirikisha shule za msingi za mjini na za vijijini. Jumla ya shule mbili zilishirikishwa. Sababu za kuteua sampuli hizi mbili za shule ilikuwa ni kushirikisha wanafunzi wa aina mbalimbali kadri inavyowezekana.

SURA YA PILI

2.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tuliangazia historia ya fasihi ya watoto. Kwanza kabisa tulichunguza historia ya fasihi ya watoto kijumla. Tulichunguza maendeleo ya fasihi ya watoto tangu enzi ya Kirumi na namna ambavyo swala la mwitikio wa mtoto msomaji lilishughulikiwa. Enzi ya kati (500-1500 B.C.E) vilevile ilichunguzwa katika hatua hii ya kwanza ya enzi ya kale.

Hatua ya pili ya kuchunguza fasihi hii ya watoto ilikuwa enzi ya kuchipuka upya kwa bara Ulaya (1500-1650). Fasihi ya watoto katika karne ya 17-19 ilichunguzwa katika hatua hii vilevile. Aidha swala muhimu ambalo tulikuwa tukichuguza ni namna ambavyo wazalishaji wa fasihi ya watoto walishughulikia swala la mwitikio wa mtoto wa msomaji katika kipindi hiki.

Hatua ya tatu tuliyoichunguza fasihi ya watoto ni ile enzi ya utawala wa Malkia Victoria (1837- 1901). Kipindi hiki kilishuhudia kunawiri zaidi kwa fasihi ya watoto. Nia yetu hasa ilikuwa ni kuchunguza iwapo kunawiri huku kulitilia mwitikio wa mtoto msomaji maanani. Aidha katika hatua hii vilevile tulichunguza fasihi ya watoto katika karne ya 20.

Baada ya kuchunguza hatua hizo tatu muhimu tuliichunguza fasihi ya watoto nchini Kenya katika vipindi vitatu. Vipindi vyenyewe vilikuwa, kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Swala kuu tulilochunguza katika hatua hizi ni namna ambavyo mwitikio wa mtoto msomaji ulivyoshughulikiwa.

Mapitio ya maandishi kuhusu mada ya utafiti yalishughulikiwa katika sura hii vilevile. Historia fupi ya Ken Walibora ilituangazia kuhusu maisha, mtazamo na tajriba ya mwandishi ambaye vitabu vyake vilishirikishwa katika utafiti.

Ufafanuzi wa Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ulipatikana katika sura hii.

2.2 Historia ya Fasihi ya watoto

2.2.1 Enzi ya kale ya Kirumi (50 B.C.E-500B.C.E)

Fasihi ya watoto imepitia hatua mbalimbali za ukuaji. Hatua hizi zilianza enzi ya kirumi (50 B.C.E) hadi kufikia sasa. Katika enzi hii, fasihi ya watoto haikuandikwa. Ilitungwa ili kusikizwa tu. Watoto katika kipindi hiki walipokea fasihi yao kupitia wasimulizi waliokomaa. Kipindi hiki kilikuwa na kazi chache za fasihi ya watoto. Watoto walisikiza fasihi ya watoto kama vile ya *Homer, The Iliad, The Trojan war, The Odyssey*. Kwa mujibu wa Oberstein, K. (1994), katika kipindi hiki watu waliokomaa walivutiwa na fasihi ya watoto pia hasa iliyokuwa na maudhui ya kimapenzi. Watoto kwa upande wao walivutiwa na kazi zilizokuwa na mambo ya ajabuajabu, ziara za kitambuzi, majitu. Hadithi za Esopo vilevile zilikuwa pendwa kwa watoto wengi.

Hata ingawa kipindi hiki kazi zilizoandikwa ziikuwa nadra kupatikana, hatujaelezwa endapo mtambaji alichunguza miitikio ya watoto wasikilizaji alipokuwa akisimulia hadithi. Mtoto hakupewa nafasi ya kusema ni hadithi gani ilikuwa mwafaka kwake. Msimulizi alisimulia tu chochote alichokuwa nacho bila kujali umwafaka wake kwa mtoto msikilizaji.

2.2.2 Enzi ya Kati (500- 1500 B.C.E)

Ni watoto wachache tu walioweza kusoma katika kipindi hiki katika bara Ulaya. Hivyo basi ni kazi chache tu zilizoandikwa kwa ajili ya watoto. Katika kipindi hiki, watoto hawakupewa nafasi tosha ya kujieleza. Chochote walichosema kilidharauliwa. Mara nyingi kazi zilizoandikwa zililenga hadhira iliyokomaa pia. Kwa mujibu wa Lesnik-Oberstein, K. (1994), miongoni mwa kazi zilizoandikwa katika kipindi hiki ni *Beowulf, Song of Roland pamoja na Elcid.* Watoto katika kipindi hiki walivutiwa na kazi zilizokuwa na maudhui ya kimapenzi vilevile. Lesnik-Oberstein, K. (1994) anaendelea kutoa mifano ya kazi hizi kama vile, *King Arthur and his Knights of the Round table* (karne ya 12-13), *Robin Wood* miongoni mwa kazi nyingine.

Simulizi zilizowavutia watoto hasa ni zile za Kirumi. Kazi hizi zilisheheni utamaduni wa Warumi. Hadithi za wanyama zilikuwepo pia katika kipindi hiki. Pia kulikuwepo na hadithi za Biblia. Mifano ya hadithi za Biblia ni hadithi za watakatifu ambazo ziliwasisimua watoto walipozisoma. Aidha kwa mujibu wa hadithi walizosimuliwa watoto zilihusu ulimwengu halisi na ule usiokuwa halisi pia. Wasimulizi walijumulisha mambo ya ajabu ajabu na maghani katika usimulizi wao (Oberstein, K. :1994). Nyingi za hadithi hizi zilikuwa na maswala ya kimiujiza; hali iliyofanya fasihi hii kuleta mawazo ya kitoto bongoni mwa watoto wasomaji. Kipengele hiki kilikuwa muhimu sana katika kuwaburudisha watoto wasomaji.

2.2.3 Enzi ya kuchipuka upya kwa bara Ulaya (1500-1650)

Kipindi hiki kilishuhudia kutolewa kwa machapisho ya kwanza ya vitabu vya watoto. Hali hii ilifanya fasihi ya watoto kuenea pakubwa. Katika kipindi hiki elimu

ilienea kwa haraka sana. Huu ndio wakati Ulaya ilifika maeneo ya Marekani na kuanza biashara na ukuzaji uchumi. Wafanyibiashara waliothamini elimu walizuka katika kipindi hiki.

Kwa mujibu wa Hunt, P. (1996;102) kipindi hiki, watoto walikuwa na uwezo kiasi wa kusoma na kufahamu ikilinganishwa na hali ilivyokuwa hapo awali. Kazi nyingi zilizoandikwa katika kipindi hiki zikuwa za kuelimisha. Mfano wa hadithi hizi ni Hadithi za Esopo. Kazi nyingine zilizokuwepo katika kipindi hiki ni *Books of Martyrs (*Foxe J. *1563),* zilizokuwa zikipinga Ukatoliki. Hizi zilizopinga Ukatoliki zilikuwa na maonyesho ya kushangaza ya vifo kwa ajili ya kutetea dini. Kitabu cha mwanzo kabisa kilichopendwa na watoto wa Ulaya kilikuwa *Latin through pictures (Orbis Sensulium pictus 1568)* cha Kilatini kilichoandikwa na Comenius (1568). Mwishoni mwa karne ya 17 mabadiliko ya kijamii yalionyesha bayana kwamba fasihi ya watoto ilikuwa ikiendelea kukua.

Hata ingawa elimu ilienea kwa haraka katika kipindi hiki, Hunt, P (mtaje), anaarifu kwamba kazi nyingi zilizoitwa fasihi ya watoto zilikuwa zinalenga hasa watu wazima. Maudhui kama vile, kupinga ukatoliki, na vifo kwa ajili ya kutetea dini huenda yalikuwa mazito kwa mtoto msomaji. Licha kwamba kazi nyingi zilikuwa za kuelimisha, mwitikio wa mtoto msomaji haukutumiwa kumchagulia mtoto fasihi iliyokuwa mwafaka.

2.2.4. Karne ya 17.

Katika kipindi hiki, Lesnik-Oberstein (mtaje) anatambua kwamba watoto walianza kutiliwa maanani zaidi. Watu waliokomaa walianza kutambua haja za watoto na namna ambavyo wanaweza kuzikidhi kupitia kazi zilizoandikwa. Mihemko miwili

iliyochangia pakubwa katika kumshughulikia mtoto ilikuwa ile ya kidini na ile ya kiuwezo-akili.

Mhemko wa kidini, ulikita mizizi katika Biblia takatifu. Kilichopigiwa debe hapa ni ujuzi wa kujua kusoma na kuifahamu Biblia. Kwa njia hii, ilitarajiwa kwamba wasomaji wangeiamini dini na kuweza kuupalilia wokovu waliopata. Chuo kikuu cha Havard kilianzishwa mwaka wa 1636 ili kutoa mafunzo ya dini. Fasihi ya watoto vilevile ilitarajiwa itokane na hadithi zilizokuwa katika Biblia. Hati za Kirumi zilitumika pakubwa katika kuanisha fasihi ya watoto. Kwa mfano, hadithi zilizokuwa na anwani iliyoanza kwa 'A' basi ziliwekwa pamoja. Mifano ya hadithi ni A: Adamu alianguka hivyo tukawa wenye dhambi.

Mhemko wa pili ulizuliwa na mwanafilosofia Mwingereza John Locke. Mwakani 1693, John Locke (mtaje) aliandika makala maarufu kuhusu elimu ya mtoto. Alionyesha kwamba akili za mtoto ni kama kitabu kisicho na maandishi (tabula rasa) na kilichosubiri kuandikwa. Aliamini kwamba kila mtoto alikuwa na uwezo wa kusoma na kwamba lilikuwa jukumu la watu waliokomaa kuhakikisha kwamba watoto wao wanapata elimu njema. Ni muhimu nitaje kwamba katika kipindi hiki fasihi ya hadhira iliyokomaa ilikuwepo kwa wingi na kwa kiasi fulani iliwavutia watoto pia. Mifano ya kazi za Swift J.(1906) zilikuwa kama vile *Gullivers Travels.*

Katika karne hii, tuligundua kwamba mtoto vilevile hakushirikishwa katika uzalishaji wa fasihi ya kidini aliyoandikiwa na mwandishi aliyekomaa. Ilichukuliwa kwamba mradi fasihi yenyewe ilitokana na Biblia takatifu basi sharti iwe mwafaka kwa mtoto msomaji. Vilevile, tafiti zilizokuwa zinafanywa na Locke,J.

(1693) zilikuwa za kuwapotosha wazalishaji wa fasihi ya mtoto. Dhana kwamba akili ya mtoto ni kama kitabu kisichokuwa na maandishi kinachoweza kuandikwa chochote huenda ilichangia pakubwa katika kuzalisha fasihi ya watoto ambayo haikuwa mwafaka.

2.2.5 Karne ya 18 na 19

Kipindi hiki kama anavyosema John Newberry kilishuhudia uchapishaji wa kitabu *Little Pretty Pocket Book.* (Newbery, J.1744). Inadaiwa kwamba hiki ndicho kilikuwa kitabu cha kwanza dhahiri cha fasihi ya watoto. Kilikuwa na nyimbo, hadithi zenye maadili, picha miongoni mwa zingine. Rousseau kwa upande wake anasema kwamba katika kipindi hiki, fasihi ya watoto ilisheheni maadili. Katika Emile (1762), Rousseau anasema fasihi ya watoto ililenga kukuza maadili kama vile ya kuishi vyema katika jamii. Aidha, uandishi wa vitabu vya watoto ulichukuliwa kuwa kazi duni ukilinganishwa na uandishi wa fasihi ya watu wakomavu. Hali hii ilipelekea wanawake kujitoma katika fani hii ya kuwaandikia watoto.

Kipindi hiki kilishuhudia kuibuka kwa simulizi. Hadi kufikia karne ya 19, ilikuwa vigumu kuainisha fasihi ya watoto. Mifano ya kazi katika kipindi hiki ni *Tales of mother goose* na Parrault, C. (1696), *Cinderella,* Parrault, C. (1697). Karne nzima ya 18 ilishuhudia kusimuliwa upya kwa hadithi za kale. Mwanzoni mwa karne ya 19 kulikuwa kazi ya *Grimm Brothers* (Grimm J. na Grimm W. 1885). Ni muhimu kutaja kwamba, simulizi hazikuchukuliwa kuwa fasihi ya watoto kwa ujumla wake. Kuna watu wakomavu waliopendekeza kwamba simulizi hizi hazifai kamwe kwa watoto. Sababu ikiwa ni kwamba zilikuwa na maudhui ya watu wazima kwa mujibu wa Hunt(mtaje).

Baadhi ya maudhui haya yalikuwa uwazi uliotisha, vita na zaidi hazikuwa na maadili kwa mtoto. Hata hivyo, watoto waliendelea kuzisoma na kuzipenda.

Katika kipindi hiki, tulikumbana na vuta nikuvute kati ya mhakiki na mtoto msomaji. Mhakiki aliyekomaa alijaribu kutoa maoni akisema kwamba fasihi ya watoto iliyokuwepo haikustahili kusomwa na watoto kamwe. Sababu ikiwa kwamba kazi zile zilikuwa simulizi-kale na kwamba zilikuwa na maudhui mazito kwa mtoto msomaji. Kwa upande wa mtoto, Hunt (mtaje) anaendelea kutuarifu kwamba mtoto aliendelea kusoma na kuzipenda kazi hizi licha ya mhakiki aliyekomaa kupendekeza kwamba hazifai. Linalotokeza bayana hapa ni kwamba, mhakiki aliyekomaa alijaribu kumchagulia mtoto fasihi bila kumshirikisha. Aidha tumetaja hapo awali kwamba sio lazima anachokiona mhakiki aliyekomaa kuwa ni mwafaka kwa mtoto kiwe ni mwafaka kwa mtoto msomaji.

2.2.6 Enzi ya Malkia Victoria.

Hii ilikuwa enzi ya utawala wa Malkia Victoria (1837-1901); Kipindi ambacho fasihi ya watoto ilinawiri zaidi kote ulimwenguni. Fasihi ya watoto katika kipindi hiki iliathiriwa na wimbi la fasihi pendwa ambalo lilipelekea kuwepo hamu kubwa ya fasihi ya watoto. Waandishi shupavu na wachoraji walianza kuonyesha na kuwekeza vipawa vyao katika watoto na fasihi yao.

Katika fasihi ya kimazingaombwe (fantasies) Carrol, L. (1865) aliandika kitabu kilichokuwa na anwani *Alice's adventure in Wonderland* kilichochapishwa na Dodgson math Proof Oxford. Kitabu hiki kilizua enzi mpya kuhusiana na fasihi ya mtoto. Ilikuwa enzi ya kuchapishwa fasihi ya mtoto ambayo ilikwepa elimu au maudhui muhimu. Fasihi hii ililenga kuburudisha mtoto pekee.

Mifano ya fasihi iliyolenga wavulana ilikuwa Stevenson's *Treasure island* (1863); Watoto Waingereza walivutiwa na fasihi yenye mazingira tofauti na yale ya Uingereza. Wamarekani nao walivutiwa na fasihi ile iliyosawiri mazingira ya Marekani. Novela ambazo hazikuzingatia kanuni za fani zilikuwa kochokocho. Baadhi ya fasihi hizi za shuleni zilijiri karne ya 20.

Fasihi ya kinyumbani katika kipindi hiki ililenga wasichana. Hadithi zilizoonyesha wasichana waliofanikiwa maishani zilikuwa tele. Baadhi ya maudhui yalikuwa furaha ya mwanamke katika ndoa. Kwamba wanawake walistahili kuwapenda waume zao ili waweze kufurahia maisha ya ndoa. Mifano ya kazi hizi ilikuwa ni *Little Women* na Alcott's (1868)

Katika kipindi hiki, fasihi ya watoto haikuwa na picha wala michoro mingi. Wachoraji hawakuwa wametambua siri hii ya kuweka picha katika fasihi ya watoto. Hata hivyo kama anavyodai Lesnik-Oberstein (mtaje) mwishoni mwa karne ya 19, mabadiliko katika uchapishaji na uandishi yalivutia wachoraji wengi kiasi kwamba fasihi ya watoto yenye michoro ilianza kujitokeza sokoni kwa bei nafuu.

Katika robo ya kwanza ya karne ya 20, maktaba zilianza kutenga sehemu za fasihi ya mtoto. Hatua kubwa ilikuwa imepigwa kuhusiana na fasihi ya watoto.

2.2.7. Karne ya 20: Kutanuka kwa ulimwengu.

Katika kipindi hiki, kumekupo machapisho anuwai ya fasihi ya watoto. Hunt P.(mtaje), Miongoni mwa haya ni machapisho ya picha, mashairi, mambo ya ajabuajabu, machapisho halisia na yale ya kuelimisha. Kutambuliwa kwa ubora wa fasihi ya watoto

kumekuwepo. Zawadi zilitolewa kwa machapisho yaliyokuwa bora zaidi. Marekani kwa mfano ilkuwa na tuzo zifuatazo;

(i) Medali ya Newberry kwa kitabu cha fasihi ya watoto kilichokuwa bora zaidi.

(ii) Medali ya Caldett kwa aliyechangia zaidi katika uchoraji picha za fasihi ya Watoto kama inavyooonekana katika tovuti ifuatayo; 2007 Literary and Related Award Winners.

2.3 Fasihi ya watoto nchini Kenya.

Fasihi ya watoto nchini Kenya imepitia hatua mbalimbali. Odaga (1985) anasema kwamba hatua hizi ni tatu. Fasihi ya watoto kabla ya ukoloni, fasihi ya watoto enzi ya ukoloni na fasihi ya watoto baada ya ukoloni. Hatua zote hizi zimeathiri fasihi ya watoto pakubwa kwa njia mbalimbali.

Fasihi ya watoto kabla ya ukoloni, ambayo ilikuwa simulizi ndiyo kongwe zaidi nchini Kenya na barani Afrika kwa jumla. Fasihi simulizi imekuwepo hata kabla ya maajilio ya maandishi (Finnegan, R.1970). Fasihi simulizi ilikuwa mojawepo ya taasisi muhimu katika utamaduni wa Mwafrika. Fasihi hii ilijumlisha tanzu kama vile nyimbo, methali na vitanza ulimi. Tanzu zote hizi zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutumia mdomo. Fasihi hii ilisheheni filosofia ya jamii mbalimbali za Kenya kando na kuwa chombo cha kuelimisha. Watoto walijua kujiheshimu na kuheshimu wengine kupitia fasihi hii. Aidha, fasihi hii ilitumika pia kama chemichemi ya burudani. Burudani ilipatikana kutokana na maudhui na utendaji wa msimulizi. Aidha ni kutokana na utendaji kwamba fasihi simulizi haikusahaulika miongoni mwa wanajamii. Scheub (1977)

anasema kwamba utendaji katika utambaji hadithi ulikuwa na maana ya ndani na ulidhamiriwa kupitisha ujumbe fulani kwa watoto wasikilizaji.

Fasihi ya watoto kabla ya ukoloni haikuthaminiwa tu kwa sababu ya nafasi yake katika jamii na uthamana wa utendaji uliokita ndani yake mbali umbuji wake uliwavutia na kuwashika wengi. Fasihi hii ilikuwa na vipengele mbalimbali vya kuvutia; kwa mfano ilikuwa na lugha ya kishairi ambayo iliteka mäkini ya mtoto msomaji vizuri. Msanii mtambaji vilevile alitumia mbinu za lugha ambazo ziliongeza thamani ya simulizi. Mbinu za lugha hizi hazikuwa pale tu kuhakikisha kwamba mtoto anakumbuka funzo analolipata katika hadithi mbali pia kumpa burudani.

Maajilio ya wakoloni yallipelekea fasihi simulizi kupoteza dhima yake ya kuwa chombo cha kufunza watoto. Nafasi yake ilianza kunyakuliwa na fasihi ya watoto ya kigeni. Kwa njia hii, fasihi simulizi ya Wakenya ilianza kupewa nafasi ya pili polepole huku watu wakibugia elimu iliyoletwa na mkoloni. Fasihi ya kigeni ikaanza kutumika kama chombo cha kupitisha elimu. Fasihi ya kikoloni ni ile ambayo iliandikwa kwa ajli ya mzungu kisha Wakenya na Waafrika wengine kwa jumla wakalazimishwa kuijua. Fasihi hii ya kikoloni ililenga kuonyesha 'ujinga' wa Mwafrika na ilitumika kuwaonyesha wazungu kwamba hakukuwa tofauti kati ya Mwafrika na mnyama. Mwafrika aliyetambulishwa kwa fasihi hii ya kikoloni alijiona duni baadaye kutokana na uongo uliofukiziwa fasihi yao. Aidha msomi wa Kiafrika aliyetambulishwa kwa fasihi hii, aliishia kujidharau na kuugua ugonjwa ulioitwa na Okot p' bitek (1973) "Unyani". Ugonjwa huu uliwafanya Wakenya na Waafrika kwa jumla kujidharau na kujaribu kuwaiga wakoloni ili waitwe 'wastaarabu' na wakubalike kwa urahisi katika vikao vya wakoloni.

Maajilio ya uhuru hayakubadili mambo. Fasihi ya watoto ya kikoloni iliendelea kuwa pamoja na ile ya baada ya ukoloni. Hata hivyo vuguvugu la kukataa ile ya kikoloni ilianza. Thiong'o (1981) na Okot p' bitek (1973) ni miongoni mwa wale waliopendekeza kuwe na mabadiliko. Hata hivyo katika kipindi hiki kulikuwa na vitengo vitatu vya fasihi ya watoto. Kitengo cha kwanza kilikuwa fasihi ya kikoloni ambayo tumekwisha taja kwamba ilikuwa na athari za kisaikolojia kwa mtoto wa kiafrika. Pili kulikuwepo fasihi ya watoto ya kilimbwende ambayo haikutoa picha halisi ya nchi ya Kenya au bara la Afrika kwa jumla. Aidha fasihi hii iliandikiwa Wakenya/Waafrika na wasanii ambao hawakuwa Wakenya/Waafrika. Tatu, kulikuwa fasihi iliyoandikwa ili kutoa picha halisi ya Mwafrika. Hii iliandikwa na Waafrika ambao nia yao ilikuwa kutoa picha potovu ya Mkenya/Mwafrika iliyokuwa imeingizwa katika fasihi. Walitaka kuandika fasihi ya watoto upya ili ionyeshe picha halisi ya Mkenya/Mwafrika na kudumisha hadhi yake. (Odaga 1978: 44) Sababu hii ndiyo ilifanya kuwe na kasi ya uandishi wa fasihi ya watoto kwa Kiingereza na Kiswahili kuanzia mwongo wa 60 hadi hivi leo, Fasihi ya watoto katika kipindi hiki ilikuwa na umuhimu kwa mtoto. Ilijaribu kumfanya mtoto ajitambue yeye mwenyewe bila kumsukumia maswala ya mtu mzima. Hali hii ya mtoto kujitambua imechangiwa hasa na tahakiki mbalimbali za fasihi ya mtoto ambazo zimekuwepo.

Utafiti uliofanywa na Kitonga (1984) kwa mfano, ulionyesha kwamba uchapishaji wa fasihi ya watoto kwa lugha yoyote ile hutokea tu endapo soko la vitabu vile litakuwepo. Taasisi ya elimu nchini Kenya ndiyo huwa soko kuu hasa lakini si vitabu vyote vinavyoidhinishwa na Taasisi ya Elimu kutumika shuleni. Hali hii imekuwa kikwazo katika kuendelea kwa fasihi ya watoto. Shida nyingine ni kwamba hata ingawa makampuni ya uchapishaji yameanza kuchapisha vitabu vingi, wazazi wachache hununua

vitabu hivi. Wazazi walio na uwezo wa kununua ambao ni wachache, wana watoto ambao hawana hamu ya kusoma vitabu maanake wakati wao mwingi hutumiwa kwa shughuli nyingine za kujistarehesha. Kwa walio na uwezo kadri wa kifedha, ni adimu kwa watoto wao kusoma fasihi ya watoto. Kitonga, E (1984:93) anasema kwamba hali hii inatokana na ukosefu wa fedha za kununua baadhi ya vitabu hivi. Ununuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto vitakavyowasaidia watoto kupita mtihani ndio mtindo umekuwepo kwa muda mrefu.

Licha ya vikwazo hivi, kuwepo juhudi za kuikuza fasihi ya watoto kumeanza kuonekana. Wasanii na wachapishaji wamejitokeza kuikuza fani hii. Aidha, hapo awali, fasihi ya watoto kwa Kiingereza ndiyo ilikuwa ikitambulika zaidi. Mifano ni fasihi ya watoto na Kimenye, B. (1967): Mfano mmoja ukiwa *Moses and the mildred.* Hivi sasa wasanii wamejitoma uwanjani kuwaandikia watoto kwa Kiswahili. Akina Kitula King'ei, David Maillu, Ken Walibora, K.W. Wamitilla wamo mbioni kuhakikisha kwamba mtoto anayo fasihi ya watoto kwa Kiswahili. Aidha hali hii imepelekea kutambuliwa kwa utanzu huu kama kitengo cha elimu kinachojitegemea. Juhudi hizi za kuimarisha fani ya utanzu huu italeta kasi mpya katika usomaji wa fasihi ya watoto miongoni mwa watoto.

Katika historia ya fasihi ya mtoto nchini Kenya, Odaga (1978:61) anaendelea kusema kwamba malumbano kati ya waandishi wenyeji na waandishi wa kikoloni ndiyo yalikita katika fasihi ya watoto. Vipindi vyote vitatu havikuzalisha fasihi ya mtoto iliyolenga mtoto kujitambulisha na kipindi cha utotoni. Mkoloni alitaka mtoto kutojitambulisha na Waafrika wenzake; yaani kumkengeusha. Akina Thiong'o (1982) nao walitaka kuonyesha mtoto kwamba mkoloni ni kiumbe kilichostahili kupuuzwa kabisa. Katika vuta nivute hii, basi umbile jumla la fasihi ya watoto likaathirika. Mtoto

akasukumiwa kusoma yale ambayo labda hayataki na hayamfai kamwe maanake hawa wote hawakuchunguza jinsi ambavyo mtoto aliitikia kazi walizomwandikia.

2.4 Dhima ya fasihi ya mtoto

Kwa mujibu wa Hunt (1992:76) fasihi ya watoto inawawezesha watoto;

(1) Kuwa na hamu ya kujitambua wao ni akina nani.

(2) Kuulewa ulimwengu halisi.

(3) Kuwajua watu na sehemu mbalimbali

(4)Kuielewa mitambo mbalimbali ya kitekinolojia na jinsi inavyofanya kazi.

(5) Kuwa na hamu ya kujua mambo yalivyo na jinsi ya kuyathibitisha

(6) Kutambua vipengele wanavyotumia binadamu ili kuishi.

(7) Kuwawezesha watoto kuwa wabunifu.

(8) Kujua namna ya kuishi na binadamu wengine katika jamii

(9) Kutambua mifumo ya kisayansi na kuweza kuiamini

(10) Kuwa na hamu ya kuujua ulimwengu razini.

Takribani dhima zote hizi za fasihi ya watoto zinadokezea umuhimu wa mwitikio wa mtoto msomaji. Hivyo basi, ipo haja kubwa ya kufanyia utafiti mwitikio wa mtoto msomaji.

2.5 Mapitio zaidi ya maandishi- Tasnifu.

Akimnukuu Nina Bawden, Lesnik-Oberstein, K. (1994) anasema kwamba washikadau wengi wamekuwa wakimchukulia mtoto kama kifaa kisichokuwa na akili

wala kisichoweza kutoa maoni. Walidhani kifaa hiki kinafaa kuthibitiwa na kuchaguliwa vilivyo 'safi' bila hata kupewa nafasi ya kutoa maoni na kusikizwa. Utafiti wake ulitilia mkazo haja ya kufanyia utafiti mwitikio wa mtoto msomaji anapochagua na kusoma fasihi aliyoandikiwa na mtu mzima.

Akichunguza tamathali za usemi katika fasihi andishi ya watoto, Mwanzi (1982) aligundua kwamba watoto walikuwa na miitikio mbalimbali waliposoma fasihi ya watoto kutoka Ulaya, ya Kikoloni, na ile ya waandishi kutoka Kenya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Katika utafiti wake, aligundua kwamba watoto wasomaji walipenda zaidi wahusika weupe katika fasihi kutoka Ulaya na zile za kikoloni. Wahusika weupe walifuatiwa na wahusika chotara. Watoto waliwapenda wahusika weusi kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na wahusika weupe na wahusika chotara. Swala la wahusika ni mojawepo ya vipengele muhimu ambavyo nilishughulikia katika utafiti wangu. Hivyo basi utafiti wake Mwanzi ulitilia mkazo haja ya kutilia maanani swala la wahusika wa vitabu vitatu vilivyoshirikishwa katika utafiti. Hata hivyo, mwanzi hakutaja iwapo deta aliyopata ingetumika kuchunguza umwafaka wa vitabu vitatu vilivyoandikwa na Ken Walibora.

Lubbock (1957: 40) anasema kuwa kitabu kizuri kitajulikana bayana na hadhira lengwa. Kwamba, umbo lake na yaliyomo huenda sambamba. Kwamba haya mawili hayawezi kutenganishwa katika fasihi ya mtoto. Mawazo haya yake yatakuwa muhimu katika utafiti huu. Yaliyomo nayo yanastahili kuwa na uyakinifu. Fasihi ya mtoto inastahili kumpa mtoto burudani na vilevile kumwadilisha. Anaendelea kusema kwamba mtoto ataridhishwa na kitabu kilichoumbwa na kuandikwa vizuri tofauti na kile ambacho umbo lake sio sawa na hakikuandikwa vizuri. Hapa Lubbock (Mtaje) hakutaja mtoto

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

anaweza kuridhishwa na vipengele gani. Nitasonga mbele kuchunguza vipengele kama vile wahusika, maudhui, hati, picha, kiwango cha lugha, jalada na anwani; vipengele vinavyostahili kumridhisha mtoto anaposoma vitabu vya fasihi ya watoto.

Ray (1970) akinukuliwa na Akoleit (1990: 48) anasema kwamba watoto watapenda kazi ambazo zitaleta mazingira ya kiziara ziara na zinazowaburudisha. Anasema kwamba mwandishi yeyote yule wa fasihi ya watoto atapendeka endapo kazi yake itawaburudisha watoto wanapoisoma. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa fasihi mbalimbali ya watoto itawafurahisha watoto wa viwango mbalimbali. Ray (Mtaje) hakutaja ni vipengele vipi vinavyomfurahisha mtoto. Utafiti wangu ulidhamiria kuvitaja vipengele hivi na kuvichunguza jinsi ambavyo viliitikiwa na mtoto msomaji.

Katika utafiti wake kuhusu mwitikio wa mtoto msomaji, Akoleit (1990: 59) aligundua kwamba watoto walikuwa na miitikio mbalimbali kwa vitabu vya mwandishi Barbara Kimenye. Kwamba, kunao wahusika waliopendwa na watoto na wengine kupuuzwa kiasi cha kutotambulika. Huyu alifanya utafiti wake kwa mujibu wa fasihi iliyoandikwa katika lugha ya Kiingereza. Mimi nilijikita katika fasihi iliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili.

Dixon (1933: 106) alishughulikia dhana , mielekeo na maoni yanayopitishwa na waandishi kwa watoto wasomaji. Alifanya hivi katika kitabu alichoandika; *Catching them young*. Alitilia mkazo zaidi lugha wanayotumia waandishi na jinsi wanavyocheza na maneno ili kuzua miitiko wanayolenga kwa watoto wasomaji. Alishughulikia kazi nne za watoto. Alitoa maoni kuhusu lugha na wahusika wa fasihi ya watoto. Aliyopata ni kwamba, dhana za kisiasa hupitishwa kwa mtoto msomaji angali mchanga kupitia fasihi ya watoto. Lugha ni kipengele muhimu ambacho utafiti huu ulidhamiria kuchunguza.

Aidha utafiti wa Dixon ulinielekeza kutokana na mbinu ambazo alitumia ili kupata deta iliyohusiana na lugha.

Mabel (1988:26), mwandishi na mhakiki wa fasihi ya watoto, anasema kwamba matumizi ya picha hupitisha ujumbe fulani kwa mtoto msomaji. Anasema kwamba picha ni lugha kwa ukamilifu wake. Akishadidia anasema kuwa:

> "Uwasilishaji wa ujumbe sio jukumu la maandishi ya hati pekee.
> Kwamba picha husheheni lugha na fasihi yake kikamilifu.
> Kwamba watoto huelewa vitabu vya fasihi vyema zaidi mwandishi anapotumia michoro. Picha huchochea vitivo vya tafkira vya mtoto kando na kumburudisha."

Anasema kwamba ili picha iwe na mantiki kwa mtoto msomaji, sharti iakisi yaliyoandikwa ili mtoto aweze kuoanisha maandishi na michoro iliyowekwa. Anasema kuwa, mbinu hizi mbili ni zao la akili moja. Anasisitiza ubora wa picha anaposema kwamba sharti impendeze mtoto. Haya yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu; hata hivyo, nilisonga mbele kuchunguza sifa zaidi zinazohitajika ili picha imridhishe mtoto zaidi. Cass (1984) anafafanua hali hii pia.

Mugo (1992:26) akifafanua umuhimu wa ubora wa hati alisema kwamba mtoto msomaji atavutiwa na hati kubwa kiasi, zinazoweza kusomeka. Alisema haya kutokana na tajriba yake katika uchapishaji wa fasihi ya watoto. Kwamba anwani ya kitabu cha fasihi ya mtoto haifai kutiwa usanii kiasi cha kutosomeka. Alitoa sababu kwamba huenda mtoto akatatizika katika kusoma ile anwani. Iwapo hati za kitabu kwa jumla hazitaweza

kusomeka mtoto atakuwa na miitikio hasi licha kwamba maudhui yaliyokita katika kitabu hicho ni muhimu kwa mtoto msomaji. Anapendekeza kwamba, hati zinastahili kuwa katika kiwango cha 12-18; kipimo cha tarakilishi. Alisema kiwango kitategemea aina ya mtoto lengwa. Kwamba ukubwa wa hati upungue jinsi umri wa mtoto unavyozidi. Alisisitiza umuhimu wa hati kukolezwa rangi ili ziweze kusomeka vyema. Alisema mtoto atakiweka pembeni kitabu ambacho hati zake hazisomeki vyema huku akipendelea kile kilichoandikwa vizuri. Utafiti wake huu ulinifaa pakubwa. Hata hivyo ulitofautiana na wangu maanake nilijikita kuchunguza miitikio ya watoto kati ya umri 12-16 wa darasa la 7 na 8. Utafiti wake Phoebe ulikuwa wa kijumla: Hakushughulikia kundi mahsusi la watoto.

Katika utafiti wake, Nyambura (1995) aligundua kwamba watoto nchini Tanzania walikuwa na miitikio mbalimbali waliposoma fasihi ya mtoto. Alitambua aina nne za miitikio ya mtoto msomaji. Kwanza ni Mwitikio-nyamavu (silent response). Hapa alitumia uchunguzi-shiriki kuchunguza miitikio ya watoto. Aligundua kwamba watoto walipoachwa huru kuchagua kitabu walichopendezwa nacho, walionekana kukimbilia kimoja na wakati mwingine kun'gan'gania huku wakipuuza vingine. Vilevile Nyambura (mtaje) alisikiza maongezi ya watoto kuhusu vitabu mbalimbali pasi wao kujua kwamba walikuwa wakichunguzwa. Aina ya pili ya miitikio iliyobainika ni usomi-wingi wa kitabu kimoja. Tatu, aligundua kwamba watoto walipoambiwa waandike upya hadithi waliyopendezwa nayo walipendelea hadithi fulani. Nne alitambua pia kwamba watoto hawa walipoambiwa waigize mchezo fulani kutokana na vitabu walivyosoma walipendelea kitabu fulani pia. Utafiti huu wake ulinisaidia katika mbinu alizotumia kutambua miitikio. Utafiti huu ulitofautiana na wangu maanake wanafunzi wangu

hawakuwa na ujuzi wowote wa vitabu vilivyokuwa vinafanyiwa utafiti. Vilevile nilishughulikia wanafunzi kutoka Kenya tofauti na yeye aliyeshughulikia wanafunzi kutoka Tanzania. Aidha wanafunzi wangu hawakuhitajika kufanya maigizo kama walivyofanya katika utafiti wa Nyambura.

Katika makala aliyowasilisha katika kongamano la fasihi ya watoto Agwu akinukuliwa na Emenyonu (1990: 68) alisema kwamba watoto kati ya umri wa miaka 11-14 walikuwa na miitikio iliyolingana kwa kiasi fulani. Kwamba wao walipenda fasihi iliyokuwa na wahusika wanyama, na iliyokuwa na mambo ya kiajabu-ajabu kama vile majitu, na vilevile fasihi iliyosawiri mazingira ya nyumbani. Alidai kwamba maswala kama vile majitu na vilevile fasihi iliyosawiri mazingira ya nyumbani ilipendeka sana na watoto. Aliendelea kudai kwamba maswala kama vile ya mapenzi na vifo yatawavutia wanaoanza kubaleghe. Michele (1993:86) vilevile aliungama kauli hii. Hivyo basi, alidai waandishi wa fasihi ya watoto nchini Nigeria hawajakuwa wakirejelea swala la hadhira lengwa ambalo kwake ni swala muhimu sana. Katika kugeza ugumu wa hadithi alipendekeza " Fry Readability Graph" pamoja na ule wa kugredi wa SMOG (SMOG Grading Formula). Mbinu hizi mbili zilimsaidia kuanisha sampuli (ya vitabu) yake kwa misingi ya ugumu wa kusomeka wa hadithi zenyewe. Aligundua kwamba sampuli aliyozingatia ilikuwa na ugumu kiasi kwa mtoto ; hivyo basi, akapendekeza kwamba vinastahili kwa mtoto wa Nigeria. Utafiti huu ulinisaidia katika uteuzi wa sampuli. Kwamba sampuli yangu ilijumlisha watoto wenye umri kati ya miaka 12-16. Utafiti wangu ulitofautiana na wake maanake katika utafiti wangu ugumu wa hadithi ulitambulika kutokana na Mwitikio wa mtoto msomaji

Katika utafiti wake, Bylan, E. (1991) aliikashifu fasihi ya watoto iliyodidimiza walemavu katika jamii. Alisema kwamba kila alipoisoma fasihi yoyote ile, wahusika walemavu walisawiriwa kama wasio na umuhimu wowote katika jamii. Alisema kwamba wanawake walemavu walisawiriwa kama wasiokuwa na hisia za kimapenzi na vilevile kama wasiokuwa na uwezo wa kujipatia marafiki. Katika fasihi ya watoto, alisema kuwa wahusika wenye macho makubwa au waliokuwa na nundu mgongoni, wafupi, wanene na waliokuwa na aina nyingine ya ulemavu walitumika kuwatisha watoto barabarani wakitoka shuleni wakielekea nyumbani. Alisema kwamba fasihi sampuli hii huibusha mwitikio hasi hasa inaposomwa na mtoto mlemavu. Mtoto mlemavu hujidharau na kujiona duni, hali inayompelekea kutovipenda vitabu hivi. Hivyo basi Bylan (mtaje) alipendekeza wahusika wanyama watumike katika fasihi ya watoto. Maoni haya yalinisaidia pakubwa katika kuchunguza mwitiko kuhusu wahusika wa vitabu. Aidha nilijikita kuchunguza mwitikio wa mtoto msomaji pekee tofauti naye aliyezingatia pia mwitikio wa mtu mzima.

Kingston (1974) alifanya utafiti wake kuhusu swala la mgogoro katika fasihi ya watoto. Aligundua kwamba, mgogoro kama ilivyo katika jamii halisi ndio hukuza fasihi ya hadhira komavu. Aidha aligundua kwamba wasomaji waliokomaa hujinabisha na fasihi waliyoandikiwa endapo ilizua mgogoro halisi kama ulivyo katika jamii. Vilevile Kingston (mtaje) alisema kwamba fasihi ya watoto ilistahili kuwa na mgogoro pia licha kwamba swala hili limekuwa likipingwa vikali sana na baadhi ya wahakiki. Kingston (mtaje) alisonga mbele kuonyesha jinsi ambavyo mgogoro uliweza kutumika katika fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali. Kwa njia hii, aliwapa wasanii wa fasihi ya watoto kielekezi wanapoiandika fasihi yao. Mtafiti huyu, alishughulikia kipengele kimoja tu;

mgogoro. Hakutumia mwitikio wa mtoto msoamaji kutambua mgogoro uliopo katika fasihi ya watoto. Tofauti na utafiti wake, utafiti wangu ulishughulikia viashiria tisa nilivyotaja hapo awali kwa misingi ya mwitikio wa mtoto msomaji.

Hunt (1992:120-124) alitambua miitiko tofauti baada ya kuwapa watoto na watu waliokomaa aina moja ya kitabu cha fasihi ya watoto wakisome. Alitumia kitabu 'Midnight' kilichoandikwa na Thomas Stow. Aligundua kwamba watoto walikuwa na miitikio iliyokaribiana kiasi kuhusu mhusika 'Midnite' aliyekuwa kondoo. Alipochunguza mwitikio wa msomaji mkomavu, palitokeza hisia tofauti kabisa. Watoto Mathew, Andrew na Rebecca; wote kutoka Australia walimpennda mhusika 'Midnite' kutokana na sifa aliyokuwa nayo ya upole pamoja na jinsi alivyotangamana na wahusika wengine. Watu waliokomaa walipoulizwa, walisema kitabu hicho hakikuwa na umuhimu wowote maanake kilihusu wanyama wakiwa msituni tu. Hii ilidhihirisha wazi kuwa mwitikio ya wasomaji hutofautiana kutegemea umri wa wasomaji. Na kwamba, maoni ya mtu aliyekomaa kuhusu kitabu fulani cha watoto hayawezi kuaminiwa asilimia mia moja. Mawazo haya yalikuwa muhimu kwangu hasa katika uteuzi wa sampuli kwamba wanafunzi niliowachagua sharti wangekuwa wa kiwango sawa.

Ilikuwa bayana kutokana na mapitio ya maandishi kwamba mwitikio wa mtoto msomaji kwa fasihi andishi ya watoto kwa Kiswahili haujachunguzwa kwa undani wake; hasa katika fasihi ya watoto iliyoandikwa na Ken Walibora. Hali hii ilionyesha kwamba kulikuwa na nafasi pana ya kuifanyia uchunguzi fasihi hii. Utafiti huu basi ulikuwa mojawepo ya juhudi zilizolenga kuchunguza fasihi hii kwa kurejelea ile iliyoandikwa na Ken Walibora.

2.6. Historia ya mwandishi Ken Walibora.

Jina kamili la msanii huyu ni Kennedy Waliaula. Jina la lakabu 'Walibora' alilibuni mwenyewe kutokana na silabi mbili za kwanza: 'Wali' kisha akaswahilisha 'aula' ambalo katika jamii ya Waluhya (jamii anamochipukia) lina maana ya 'bora'. Walibora alizaliwa miaka 40 iliyopita katika kijiji cha Sangura kata ya Cherangany Wilayani Trans Nzoia. Yeye ndiye kifunga mimba katika familia ya wavulana 4 na msichana 1.

Ken alisomea katika shule ya msingi ya St. Joseph Kitale. Alijiunga na shule ya Upili ya Koelel baada ya shule ya msingi. Baada ya kufuzu kidato cha sita, alifunza Kiswahili katika shule ya Upili ya Sitatunga. Kutoka hapo akaajiriwa kazi serikalini katika idara ya mahakama. Katika safari hii amekuwa akirudi darasani na kujiongezea elimu. Alifuzu kutoka chuo kikuu cha Nairobi na shahada katika fasihi na Kiswahili. Vilevile alifuzu kutoka chuo cha Kenya Institute of Administration na Stashahada. Hivi sasa, Waliaula yuko katika chuo Kikuu cha Ohio nchini Marekani akisomea fasihi na maswala ya Kiafrika katika kiwango cha Uzamili.

Katika maisha yake ya uandishi na Utangazaji, Ken alikuwa na ndoto ya kuwa askari polisi alipokuwa na umri wa miaka 10. Hali hii ilitokana na tajriba aliyopata wakati huo. Aliona askari polisi wakiwakamata mibabe ya watu waliokuwa wakimsumbua yeye na marafikize kila mara. Jinsi alivyoendelea kukua, ndivyo matazamio yake yalivyoendelea kubadilika. Vijijini Kitale alimokulia, alicheza mpira na kutizama runinga. Hivi ndivyo viburudisho alivyovipenda zaidi. Aliwasikiza kwa makini watangazaji Mambo Mbotela, Abdul Ngalawa na Salim Mbonde. Hawa ndio walimchochea kuingia katika ulimwengu wa utangazaji. Katika utangazaji, Ken alianzia

katika idhaa ya utangazaji KBC. Hapa alifanya kazi kama mhariri, mkalimani, na hatimaye mtangazaji wa redio na runinga. Alihamia baadaye katika kituo cha utangazaji cha Nation mwaka wa 1999. Yeye ndiye alibuni msamiati 'eneobunge' kama tafsiri ya 'constituency'.

Walibora ameandika vitabu saba: *Siku Njema , Kufa Kuzikana, Ndoto ya Amerika , Mgomba Changaraweni, Mtu wa Mvua, Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza kitabu cha Wanafunzi , na Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza Kitabu cha Mwalimu.* Falsafa na tajriba zake zilitokeza kwanza katika riwaya yake ya kwanza ya *Siku Njema.* Katika riwaya hii anawaasi wasomaji kuthamini utanashati, kutia bidii maishani, kuheshimu wanajamii wengine na vilevile kuikuza lugha ya Kiswahili. Kufikia mwisho wa mwaka wa 2008, anasema kwamba vitabu sita zaidi alivyoandikwa vitaingia sokoni. Hivi ni *'The American Dream'* tafsiri ya *Ndoto ya Amerika, Kaka Tupu, Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Nne, Diwani ya Karne, Mwongozo wa Mwisho wa Kosa, Guilty but Innocent* miongoni mwa vingine. Kadri nijuavyo kazi za Ken Walibora kama vile *Mtu wa Mvua, Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni* ni mbichi na hazijafanyiwa utafiti wowote unaohusu mwitikio wa mtoto msomaji.

2.7 Msingi ya nadharia

Nadharia ya Mwitikio wa msomaji.

Utafiti wowote ule huegemezwa kwa nadharia inayoafiki. Nadharia huongoza shughuli nzima ya utafiti hadi mwisho wake. Katika kuchunguza fasihi ya watoto, kunazo nadharia anuwai ambazo zinaweza kuelekeza na kuthibiti utafiti. Mifano ni Nadharia ya Umuundo (Propp, 1960) Mtazamo wa Ki-ishara (Symbolic Approach) (Berdelman, 1961), Umaumbo (Leech, 1966) na Mwitiko wa mtoto msomaji (Rosenblatt, 1938)

Nadharia ya Umuundo inachunguza namna ambavyo fasihi imeundwa. Mifano ya vipengele ni kama vile mpangilio wa sura na ploti. Umaumbo nao hujikita kuchunguza minofu iliyokita katika maungo yale ya kazi ya fasihi. Vipengele muhimu vinavyozingatiwa vikiwa mbinu za lugha zilizotumika na maudhui. Mtazamo wa Kiishara (Symbolic approach) nao unachunguza jinsi ambavyo kazi ya sanaa inawasaidia wanajamii kujenga maoni yao kuhusu ulimwengu na kujitambulisha na ulimwengu huo. Nadharia zote hizi zina upungufu kiasi maanake hamna moja inayomshirikisha mtoto kama mshika dau wa fasihi anayoandikiwa. Hivyo basi ilibidi utafiti huu kuegemea nadharia ya mwitikio wa mtoto msomaji kwa kuwa ndiyo iliafiki zaidi katika hatua zote za utafiti na uandishi wa tasnifu.

2.7.1 Nadharia ya Mwitikio wa msomaji.

Mwasisi wa nadharia hii ni Louise Rosenblatt . Nadharia hii ilidhihirika bayana mwaka wa 1938 alipochapisha kitabu chake cha kwanza ; *Literature as Exploration.* Baadaye ilidhihirika zaidi alipochapisha kitabu cha pili; *The Reader, theText, the Poem,* mwaka wa 1978. Fish aliendeleza mawazo yake Rosenblatt mwaka wa 1980 aliposema kwamba msomaji au kundi jamii la wasomaji, lilikuwa na mchango mkubwa katika kubuni maana ya matini. Wengine ambao wamekuwa na maoni kama haya ni wanamiundo, na wanasemiotiki. Hadi kufikia miaka ya 70, nadharia hii haikuwa imepewa hadhi ya kuwa mfumo maalum wa kuhakiki. Katika kipindi cha miaka ya 70, wanaharakati wa kupinga maongozi ya kiimla katika ulimwengu wa kiakademia ndio walipigia debe nadharia hii. Kiini cha uhakiki unaorejelea mwitikio wa msomaji ni

kudhoofika kwa msingi mkuu wa uhakiki mpya kwamba kazi iliyoandikwa haifai kuhusishwa na miktadha yake inapochunguzwa.(Wamitila (2002:146)

Hawthorn (1977[a]:67) anadokeza kuwa kile kiitwacho nadharia ya mwitikio wa msomaji ni mseto wa nadharia za kuhakiki na mikabala mbalimbali ya usomaji. Mikabala hii huangaza dhima na majukumu ya wasomaji wa matini fulani. Umuhimu wa jinsi anavyoitikia msomaji unakisiwa na kauli inayotolewa na Margaret Atwood(1982) kwamba usomaji ni mfanyiko na humbadilisha mtu. Anasema kwamba msomaji hawezi kuwa mtu yuleyule baada ya kuisoma kazi fulani. Jambo hili linamfanya msomaji kusawiriwa kama mwenye mchango mkubwa katika kuvyaza na kubuni maana ya kazi inayohusika. Wamitilla(mtaje) anasema kwamba wasomaji mbalimbali huitikia kwa njia zinazotofautiana kwa vipengele- vijenzi mbalimbali vya kazi ya fasihi iliyoandikwa kwa njia zinazotofautiana. Anatoa sababu tatu zinazosababisha hali hii kuwa hivyo;

(i) Kwamba kuna vipengele vya kimsingi katika kazi ya fasihi ambavyo huelekeza mwitikio wa msomaji.

(ii) Pili ni kwamba ipo tofauti kati ya matini iliyoandikwa na miitikio ya kibinafsi ya msomaji anayehusika. Wasomaji wamewekwa katika makundi-jamii ya kiusomi mbalimbali kutegemea vipengele kama vile umri, mandhari, utamaduni na jinsia.

(iii) Kwamba matini zinaweza kutofautiana kwa namna ambavyo zinaelekeza au kutatiza mwitikio wa msomaji husika. Hamna ufafanuzi unaoweza kusemekana ndio maana kamili ya kazi iliyoandikwa. Maana mbalimbali huzuka kadri ya jinsi wasomaji walivyo.

2.7.2 Misingi ya nadharia hii.

Kulingana na Wamitilla (mtaje), mambo yafuatayo ni misingi muhimu ya nadharia ya mwitikio wa msomaji;

(i) Msomaji wa kazi yoyote ile ana mchango mkubwa katika kubuni maana. Aidha msomaji huweza kubuni maana baada ya kuchagua na kusoma kazi iliyoandikwa. Kipengele hiki kilikuwa adhimu kwangu kwa sababu mkakati mzima wa kuchunguza miitikio ya mtoto msomaji kwa asili mia kubwa utatekelezwa na mtoto msomaji. Hivyo basi, ilibidi wanafunzi wajichagulie vitabu na kuvisoma kisha nitajua jinsi walivyobuni maana.

(ii) Wasomaji wa umri mbalimbali wana miitikio inayotofautiana. Kipengele hiki kilikuwa muhimu sana kwangu hasa katika uteuzi wa sampuli. Kwamba ilinilazimu niteue sampuli ambayo miitikio yake kwa kiasi kikubwa ililingana. Hii ndiyo sababu ya kuteua watoto wa darasa la 7 na 8 waliokuwa na umri kati ya miaka 12-16.

(iii) Kwamba tofauti za kiuana huleta tofauti katika miitikio. Swala hili lilinisaidia pakubwa katika uteuzi wa sampuli. Kwamba ilibidi nishirikishe jinsia zote mbili katika utafiti.

(iv) Kwamba miitikio ya watoto wasomaji huelekezwa kwa vipengele vijenzi vya vitabu husika. Vipengele hivi ni pamoja na, anwani ya kitabu, umbo la jalada, maudhui, msuko wa hadithi, walivyosawiriwa wahusika, hati na kiwango cha lugha. Kipengele hiki kilikuwa muhimu sana kwangu kwa njia mbili. Kwanza, ni katika ubunaji wa vifaa vya kukusanyia deta. Pili ni

kwamba kilinipa mwongozo wa kuchanganulia deta yangu. Aidha deta iliyopatikana iliainishwa kwa mujibu wa kipengele hiki.

Nilikubaliana na Benton na wengine (1985) na Davis Daiches (1969: 34) waliposema kwamba fasihi ya watoto inastahili kuwa rekodi ya shughuli za utotoni walizo nazo watoto. Hivyo basi ni muhimu kwa fasihi hii kuchunguzwa kwa kina ili kuthibitisha iwapo ni rekodi ya tajriba za kitoto.

Aidha kumbukumbu za utotoni zilizorekodiwa katika kitabu humkumbusha mtoto tu tajriba za utotoni wanazopitia watoto kwa lugha anayoielewa. Uamuzi kama huu hutokana na uchunguzi wa kazi ya fasihi kwa ukamilifu wake. Kwamba lazima vipengele vyote vinavyoitambulisha fasihi fulani kuwa ya mtoto kuchunguzwa. Ni kwa misingi hii niliamua kuzichunguza kazi za Ken Walibora kwa kutumia Nadharia ya Mwitikio wa mtoto msomaji ili niweze kuthibitisha iwapo yaliyomo ni rekodi ya shughuli za kitoto.

Nadharia hii ilinifaa pakubwa katika misingi yake. Vifaa vya utafiti vilitayarishwa kwa misingi ya nadharia hii .Deta ilikusanywa kwa misingi ya nadharia hii vilevile. Hali kadhalika deta iliyoyopatikana ilichanganuliwa kwa misingi ya nadharia hii.

2.8 Muhutasari wa vitabu

2.8.1 *Mtu wa Mvua*

Kitabu hiki kilikuwa na hadithi tatu; *Sungura Hasara, Mtu wa Mvua* na *Charo na Watoto watoro.*

2.8.1.1 *Sungura Hasara*

Hadithi hii inamhusu kijana kwa jina Fumbo Amutala. Fumbo Amutala ana hamu ya kuwa nafasi ya kwanza katika lolote lile analofanya. Hapendi kushindwa katu. Kwa

sababu hiyo anampiga mwenzie Musa kwa jiwe baada yake kufunga mabao mengi. Anatumia uongo pia ili kutambuliwa kuwa mchoraji maarufu shuleni. Anapenda kurejelewa kwa jina 'Simba' pasina kujua kwamba mbwa wengi kijijini waliitwa simba pia. Aidha anamsababishia kakake masika, bughdha, inayomfanya wapigane na Rita aliyekuwa dadake Musa.

Katika hadithi hii, vijana walisawiriwa kama waliokuwa na hamu ya kufumbua mambo mapya katika ziara zao. Wanashiriki uwindaji na kujistarehesha kwa kucheza mpira wa miguu. Kakake Fumbo aliyeitwa Masika, anatumia jina Sungura Hasara kumrejelea Fumbo kwa ajil ya tabia zake za kuleta hasara kila mara.

Ujanja wa Sungura Hasara unafikia kikomo pale mwalimu mkuu anapomuabisha mbele za wanafunzi wengine. Anagundulikana kuwa mdanganyifu na mwizi alipoiba mchoro wa kakake Masika uliomsaidia kupata kandarasi ya kuchora ukuta wa shule kutoka kwa mwalimu mkuu. Anashindwa baadaye licha ya kudai kwamba anajua kuchora.

2.8.1.2 *Mtu wa Mvua*

Katika hadithi hii, Okungu ana uwezo wa kufanya mambo ya ajabu. Kwanza, hawezi kunyeshewa na pili ana uwezo wa kusitisha mvua. Inasemekana kwamba nguvu hizi aliziridhi kutoka kwa babu yake. Okungu pia ana uwezo wa kutabiri yanayoweza kutokea siku za usoni. Kwa mfano alitabiri kwamba familia ya akina Dora ingefikwa na maafa na inatokea hivyo wanapotokea wezi na kuwaiba ng'ombe wao. Hata hivyo Okungu anafanikiwa kuwarudisha ng'ombe walioibwa kwa kutumia nguvu alizokuwa nazo. Wezi walioiba wanasalimisha silaha walizokuwa nazo pia bila kusababisha rabsha

yoyote ile. Hii inatokea baada ya babake Dora na jamii kwa jumla kushindwa kuwarudisha ng'ombe wale.

Kuja kwa Okungu katika familia ya akina Dora vilevile kunaleta bahati nzuri kwake Dora ambaye hajakuwa akienda shuleni ili aweze kuwalisha ng'ombe. Kabla ya kufika kwa Okungu, Dora alikuwa mlinzi wa mifugo kwa sababu mlinzi wao alikuwa ameondoka kwenda kumwangalia mamake aliyekuwa akiugua.

2.8.1.3 *Charo na Watoto Watoro*

Hadithi ya tatu katika kitabu *Mtu wa Mvua* ni *Charo na watoto watoro.* Hadithi hii inaangazia swala nyeti la watoto kurandaranda mitaani nchini Kenya. Charo amesawiriwa kama mdanganyifu ambaye yuko tayari kumsingizia mamake wakati wowote ule anapochelewa kwenda shule. Kila mara Charo hudai kwamba sababu ya kuchelewa shuleni ni mamake kumpa vyombo vingi kusafisha. Halima, mwalimu anayemwadhibu Charo ni mkali kwa watoto wanaochelewa shuleni. Charo anapotumwa kwenda nyumbani kumuita mamake, anaamua kupotelea mitaani badala ya kwenda nyumbani wala harudi shuleni.

Mitaani, Charo anakutana na ngenge la watoto kama yeye waliozoea maisha ya mitaani. Wanamkaribisha kwa nyama iliyooza miongoni mwa uchafu mwingine. Charo anaugua baada ya kula nyama ile. Anashtukia akiwa hospitalini mikononi mwa wauguzi. Wazazi wake wanafululiza hospitalini wanapopata habari kwamba mwana wao amelazwa hospitalini. Charo, anaomba msamaha kutoka kwa wazazi wake.

2.8.2 *Ndoto ya Amerika*

Hadithi hii ni ya kiistiari. Maana ya moja kwa moja ndiyo inalenga kumburudisha mtoto na kumpa mafunzo kadha wa kadha. Hadithi yenyewe ina maana ya ndani pia ambayo kwa kiasi ni ya kisiasa. Katika hadithi yenyewe, kijana Isaya Yano (Issa) ana hamu ya kuondoka nchini kuelekea Marekani. Amekata tamaa ya kuishi kijijini baada ya kutamaushwa na rafiki yake Madoa. Madoa ameshamuahidi kwamba atamsaidia kufika Marekani endapo tu atafanikiwa kuiota ndoto ya Amerika.

Kwa upande mwingine, watoto hawa wawili hucharazwa na mama zao kila mara kwa kuwa watovu wa nidhamu. Mama zao wote ni wajane baada ya waume zao kuaga kupitia njia mbalimbali. Wote vilevile, ni masikini nyumbani mwao uk. 5 na uk. 6. Kutokana na ukali wa mama zao, vijana hawa wanapanga njama ya kutoroka nyumbani na kukimbilia Marekani. Walikuwa kwanza wafike Nairobi kwa Rock Mwamba ambaye angefanikisha safari yao ya kwenda Marekani.

Kabla ya kuondoka kwenda Nairobi, wanamuibia, mzee Wekesa shilingi 2,300 ili wapate nauli. Rock Mwamba alikuwa jizi la kutumia mabavu na alikuwa ametoroka jela mara nyingine baada ya kukamatwa. Anafahamu lugha nyingi za ulimwengu na anazo njia anuwai za kuwahepa polisi. Isa anagundua kwamba mwenzake Madoa ni jizi pia wanapokuwa pale nyumbani mwa Rock Mwamba. Madoa na Rock Mwamba wanaondoka kwa shughuli za wizi katika mtaa wa buruburu.

Wizi wao unafikia kikomo wanapokamatwa na polisi, kuwekwa kizuizini kisha kushtakiwa kortini. Isa anaachiliwa baadaye baada ya ushahidi kutoka kijijini kwamba hakuwa na hatia. Madoa anafungwa kifungo cha miezi mitatu huku Rock Mwamba akiuawa baada ya kujaribu tena kutoroka jela.

2.8.3 *Mgomba Changaraweni.*

Kitabu hiki kinahusu msichana Alice na mvulana Chongameno. Alice, aliyelelewa katika maisha ya utashi na haiba anampenda Chongameno kupindukia. Chongameno naye aliyelelewa katika maisha ya umaskini mwingi, hayuko tayari kubugia penzi lake Alice. Anasema moyo wake hauko tayari kwa mapenzi. Chongameno ni mchungaji wa mifugo na kila mara huenda msituni kuwalisha mifugo. Kwa upande wake, Alice kila mara anajirembesha ili aweze kumvutia Chongameno.

Anaposhindwa katika hatua ya kwanza, Alice anaamua kuteketeza msitu ambamo Chongameno huwalisha mifugo wake. Moto unateketeza mali nyingi ya wanajamii. Kwa mara ya kwanza, wanakijiji wanamsingizia Chongamoneo kwamba ndiye kawasha moto. Chongameno anawekwa katika ulinzi wa polisi kwa sababu wanakijiji wlikuwa na nia ya kumwadhibu.

Chongameno hakatai uamuzi wa wanajamii kwamba ndiye kateketeza msitu hadi pale ukweli unapotambulikana kwamba Alice ndiye kasababisha maafa. Alice, anaandika barua akisema kwamba ndiye kawasha moto kisha anajiua. Wanajamii wanamuomba Chongameno msamaha kwa kumdhania mhalifu.

2.9 Hitimisho

Katika sura hii, ilidhihirika bayana kwamba tangu enzi ya kale ya Kirumi, mwitikio wa mtoto msomaji haujakuwa ukitiliwa maanani. Wazalishaji wa fasihi ya watoto katika hatua mbalimbali hawajatilia maanani swala la mwitikio wa mtoto anapoisoma kazi aliyoandikiwa. Kulingana na Odaga (1985) ni kwamba waandishi wa

fasihi ya watoto nchini Kenya hawajatilia maanani swala la mwitikio wa mtoto msomaji. Waandishi waliokomaa wamekuwa tu wakiwasukumia watoto wanayoyaona ni mema machoni pao.

Wataalamu Ray (1970), Lubbock (1957) na Nyambura (1995) wametaja kwamba mwitiko wa mtoto msomaji ni tofauti na mwitikio wa mtu aliyekomaa. Kwamba kunavyo vipengele vijenzi vya fasihi ya watoto ambavyo ni muhimu zaidi machoni pa mtoto na kwa upande mwingine uwe ni upuuzi mtupu machoni pa mtu aliyekomaa. Hali hii inatupa msukumo wa kuzichunguza kazi za Ken Walibora.

Historia fupi ya Mwandishi Ken Walibora inatupatia fununu kuhusu tajriba yake. Kama anavyosema Wamitilla (2002:17) ni kwamba mwandishi huathiriwa pakubwa na tajriba yake katika kuumba muktadha, maudhui, wahusika, lugha na vipengele vingine anapoitunga kazi ya fasihi.

Nadharia ya Mwitikio wa msomaji imeweka bayana vipengele anuwai ambavyo huathiri hadhira lengwa inaposoma kazi mbalimbali za fasihi. Vipengele hivi ni kama vile umro wa hathira, tofauti za kiuana, vipengele vijenzi vya vitabu kama vile, wahusika, maudhui, anwani, jalada miongoni mwa vipengele vingine. Vipengele hivi ndivyo ambavyo vilishughulikiwa katika shughuli nzima ya kuchunguza miitiko katika vitabu vyote vya Ken Walibora.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika shughuli nzima ya utafiti. Katika kitengo cha kwanza cha utaratibu wa utafiti, tulionyesha kilichofanyika maktabani na nyanjani.

Kitengo cha pili nacho kilituwekea wazi namna ambavyo sampuli ya wanafunzi 60 iliyoshirikishwa katika utafiti ilivyoteuliwa. Maelezo yalitolewa kuonyesha namna ambavyo sampuli hii ilivyosawazishwa ili iweze kusimamia wanafunzi wote wa darasa la saba na nane wilayani Thika.

Kitengo cha tatu kilitupa mbinu za ukusanyaji deta zilizotumika. Kilitupa maelezo kuhusu vifaa na namna ambavyo miitikio ilikusanywa kwa kutumia njiia tatu.

Baadaye sehemu iliyofuata ilitoa maelezo kuhusu jinsi ambavyo deta iliyokusanywa katika hatua mbalimbali ilivyochanganuliwa.

3.2 Utaratibu wa utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Katika maktaba nilivisoma vitabu vitatu nilivyovirejelea pamoja na makala , tasnifu, na vitabu mbalimbali vinavyoelezea fasihi ya watoto. Nilivisoma vitabu vitatu nilivyovirejelea ili kuhakikisha kwamba maudhui aliyoshughulikia mwandishi sio ya kumpotosha mtoto. Utafiti kamili ulifanywa nyanjani. Hapa ndipo deta kamili ilipopatikana. Utafiti ulifanywa nyanjani kwa sababu jumuiya lengwa ilikuwa katika shule za msingi mjini Thika.

3.3 Uteuzi wa sampuli

Shule mbili za msingi ziliteuliwa wilayani Thika. Moja ikiwa ya mjini, na ya pili ikiwa mashambani. Sababu ya kuteua makundi haya mawili ya shule ilikuwa ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wa aina mbalimbali wameshirikishwa katika utafiti kikamilifu. Wanafunzi 30 waliteuliwa kutoka kila shule. Kumi na watano wa darasa la 7 na kumi na watano wa darasa la 8. Sampuli hii ilikisiwa kwamba ingeweza kuwakilisha vizuri idadi yote ya wanafunzi wilayani Thika.Uteuzi wa wanafunzi ulikuwa wa mtabakisho. Hapa sampuli ilihitajika kusawazishwa kwa misingi ya kijinsia pia.

3.4 Mbinu za ukusanyaji deta

Uchunguzi wa miitikio ulianza tu pale wanafunzi waliruhusiwa kuchagua vitabu watakavyovisoma. Vitabu vyote viliwekwa mezani na mwanafunzi alipewa uhuru wa kuchagua viwili miongoni mwa vitatu. Kipindi cha kusoma vitabu hivyo kilitarajiwa kuchukua muda wa siku 6 kila shule. Baada ya kipindi hiki wanafunzi walipewa hojaji kujaza. (Kiambatisho A). Yaliyofuata ni mahojiano kati ya mwanafunzi na mtafiti.(Kiambatisho B)

3.5 Vifaa vya utafiti

(i) Hojaji (Kiambatisho A)

(ii) Orodha ya maswali ya mahojiano.(Kiambatisho B)

(iii) Kaseti 2

(vi) Redio rekoda

Hojaji ilitumika kuchunguza mwitikio wa mtoto msomaji kwa vipengele mbalimbali vinavyovipa vitabu hivi umbile lake. Orodha ya maswali ya mahojiano nayo ilisaidia hojaji katika ukusanyaji wa deta.

3.6 Uchanganuzi wa deta

Baada ya kukusanya deta, kiliwadia kipindi cha uchanganuzi deta. Deta iliyokusanywa kwa kutazama (hatua ya kwanza) jinsi ambavyo wanafunzi waliteua vitabu iliandikwa kiasilimia na kuwekwa katika majedwali. Hatua hii ya kwanza ilisaidia pakubwa katika kuthibitisha madhumuni ya kwanza ya utafiti; kwamba watoto walidhihirisha kwamba katika uteuzi wa vitabu waliongozwa na miitikio. Kila mtoto alichagua vitabu vilivyomridhisha.

Hatua ya pili ya ukusanyaji deta ilitumia hojaji. Hojaji hii ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya Likert. Katika mfumo huu kama wanavyoeleza Oppenheim (1966) na Ebel (1972) majibu huonyeshwa kwa kutumia vibadala vitano vinavyoonyesha kiwango cha kukubaliana au kutokubaliana. Vibadala hivyo hupewa alama 1-5 . Katika utafiti huu, vibadala vilituzwa alama kama ifuatavyo;

Nakubaliana kabisa	(5)
Nakubali	(4)
Sina uhakika	(3)
Sikubali	(2)
Sikubali kabisa	(1)

Deta iliyokusanywa kwa kutumia hojaji iliandikwa kiasilimia pia na kuwekwa katika majedwali pweke kabla ya kuwekwa katika jedwali la wastani wa miitikio. Mahojiano

yaliyonaswa yalidhihirisha kwa kijumla na kimuhutasari kitabu alichopenda mtoto kwa kujisemea yeye mwenyewe.

Mwisho kabisa, deta iliyowekwa katika jedwali la mwisho ilitumiwa kuchora grafu kwapao. Grafu kwapao hii ilikuwa muhimu katika ufafanuzi wa madhumuni ya pili ya utafiti. Madhumuni ya pili yalikuwa kuthibitisha kitabu kilichokuwa mwafaka. Katika harakati nzima ya utafiti, miitikio iliyopatikana ilianishwa kwa misingi ya nadharia niliyotaja. Aidha maelezo yalitolewa ili kufafanua asilimia zilizopatikana. Matokeo haya yalihusishwa na vitabu-rejelea vya fasihi ya watoto vilivyotumika.

SURA YA NNE

4.0 UCHANGANUZI WA MIITIKIO

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tulichanganua deta tukizingatia madhumuni yetu. Kama tulivyotaja katika sura ya kwanza, madhumuni yetu ya utafiti yalikuwa kama ifuatavyo;

(i) Kuchunguza miitikio ya mtoto msomaji anapochagua na kusoma kitabu miongoni mwa vitabu vya fasihi ya watoto.

(ii) Kubainisha umwafaka wa vitabu hivi kwa misingi ya miitikio ya watoto wasomaji.

Ili kufikia malengo haya, miitikio ilichunguzwa katika hatua tatu. Hatua ya kwanza ilikuwa katika uteuzi wa vitabu na hatua ya pili ilikuwa katika usomaji halisi wa vitabu viwili vilivyochaguliwa. Hatua ya tatu (ya mahojiano) ilikuwa kwa ajili ya kujua zaidi sababu za miitikio katika hatua ya kwanza na ya pili.

4.2 Miitikio ya mtoto msomaji katika hatua ya kwanza (Uteuzi wa vitabu)

Katika hatua hii, wanafunzi walihitajika kuchagua vitabu viwili tu. Vitabu vyote vitatu viliwekwa mezani na wanafunzi wakapewa uhuru wa kuchagua watakavyovisoma. Vitabu hivi vilikuwa vya *Mtu wa Mvua*, *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni.* Watoto walichagua vitabu kama ifuatavyo;

Jedwali 1. Miitikio katika hatua ya uteuzi wa vitabu

	Ndoto ya Amerika	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
1	√	√	
2	√		√
3	√	√	
4	√	√	
5	√	√	
6	√		√
7	√	√	
8	√	√	
9	√		√
10	√		√
11	√		√
12	√	√	
13	√		√
14	√	√	
15		√	√
16	√		√
17	√		√
18	√	√	
19	√	√	
20	√		√

21	√	√	
22	√	√	
23	√	√	
24	√		√
25	√	√	
26	√	√	
27	√	√	
28	√	√	
29			√
30	√		√
31	√	√	
32	√	√	
33	√	√	
34	√	√	
35	√		√
36	√	√	
37	√	√	
38	√	√	
39	√	√	
40	√	√	
41	√		√
42		√	√
43	√		√

44	√	√	
45	√		√
46	√		√
47	√		√
48	√		√
49	√		√
50	√	√	
51	√	√	
52	√	√	
53	√	√	
54		√	√
55		√	√
56	√	√	
57		√	√
58	√		√
59	√	√	
60		√	√
Jumla ya vitabu vilivyoteuliwa	53	39	27
Jumla ya vitabu ambavyo havikuteuliwa	7	21	33
Idadi ya vitabu	60	60	60

ambavyo vilishirikishwa katika utafiti.			

Katika jedwali 1, ilibainika kwamba kulikuwa na vikundi vitatu vya watoto kutegemea jinsi ambavyo waliteua vitabu. Kulikuwa na wale walioteua *Ndoto ya Amerika* na *Mtu wa Mvua*, wengine wakateua *Mtu wa Mvua* na *Mgomba Changaraweni* kisha wengine wakateua *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni.* Asilimia pweke za kila kitabu zilitafutwa na matokeo yake yakaonyesha dhahiri kwamba asilimia kubwa ya kitabu cha *Ndoto ya Amerika* iliteuliwa kushinda vingine. Hivyo basi, kwa njia hii tukadai kwamba miitikio ya watoto wasomaji ilikuwa ya kiwango cha juu kwa kitabu cha *Ndoto ya Amerika.* Vitabu 53 miongoni mwa vitabu 60 vya *Ndoto ya Amerika* viliteuliwa kusomwa na watoto wasomaji. Idadi hii ya vitabu ilipowekwa katika viwango vya asilimia ilikuwa 88.33. Asilimia 11.67 ya kitabu *Ndoto ya Amerika* haikuchaguliwa. Kilifuatia kitabu cha *Mtu wa Mvua* ambacho vitabu 39 miongoni mwa vile 60 vilivyoshirikishwa katika utafiti viliteuliwa. Idadi hii ilikuwa 65% ilipowekwa katika viwango vya asilimia. Hivyo basi asilimia 35 ya kitabu *Mtu wa Mvua* haikuchaguliwa. Idadi ndogo ya kitabu *Mgomba Changaraweni* iliteuliwa. Vitabu 27 tu miongoni mwa 60 vilivyoshirikishwa katika utafiti viliteuliwa. Aidha idadi yake ilikuwa asilimia 43.33. Asilimia 56.67 ya kitabu *Mgomba Changaraweni* haikuchaguliwa. Jedwali lifuatalo lilitupa muhutasari kiasilimia wa namna ambavyo vitabu viliteuliwa;

Jedwali 2. Asilimia katika uteuzi wa vitabu

	Ndoto ya Amerika	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Asilimia ya vitabu vilivyoteuliwa	88.33%	65%	45%
Asilimia ya vitabu ambavyo havikuteuliwa	11.64%	35%	55%
Jumla ya asilimia	100%	100%	100%

4.3 Uchanganuzi wa miitikio iliyokusanywa kwa kutumia hojaji

Katika hatua hii, mbinu ya Likert ilitumika kutambua miitikio ya watoto baada ya kusoma vitabu viwili walivyoviteua katika hatua ya kwanza. Mbinu ya Likert kama tulivyotaja katika sura ya kwanza, ilipima deta kwa kutumia viwango vitano (Nakubaliana sana; Nakubaliana; Sina Uhakika; Sikubaliani na Sikubaliani Kabisa.) Katika hatua hii, miitikio ya wanafunzi ilikusanywa kwa kutumia hojaji ambazo zilizingatia mbinu ya Likert. Miitikio ya wanafunzi kwa vipengele mbalimbali ilikuwa kama ifuatavyo;

4.3.1. Maudhui/Mafunzo.

Baada ya kuwahoji wanafunzi kuhusu maudhui mbalimbali katika vitabu, wengi walitaja kwamba walifurahishwa na vituko vya wahusika Charo, Dora na Fumbo. Hawa wote walikuwa katika kitabu cha *Mtu wa Mvua*.Walikumbwa na masaibu mbalimbali

ambayo ndiyo masaibu halisi ambayo yaliwakumba watoto wasomaji katika jamii. Maudhui ya ziara (kuwinda kwa kutumia mbwa), ujinga wa mhusika Fumbo, uchezaji wa mpira wa miguu (lifundo), vita vya watoto na maswala ya ajabu ajabu *(Mtu wa Mvua)* ndiyo yaliyowavutia wanafunzi wengi. Wanafunzi waliweza kuuona ulimwengu wao halisi zaidi katika kitabu cha *Mtu wa Mvua.* Wengi walijinasibisha na maudhui ya kitabu hiki kiasi cha kutoa mifano katika maisha yao iliyoshabihiana na maudhui katika kitabu cha *Mtu wa Mvua.*

Kwa uyakinifu, hadithi ya *Mtu wa Mvua* iliambatana na maswala ya ajabu ajabu (fantasy) ambacho ni kipengele muhimu sana kwa wanafunzi wa umri mdogo. Kitabu cha *Mtu wa Mvua* kilikuwa na mafunzo mengi kwa watoto wasomaji kuliko vitabu vile vingine viwili. 70.76% ya wanafunzi waliosoma kitabu cha *Mtu wa Mvua*, walisema kwamba kitabu hiki kiliwapa mafunzo mengi kuliko kile kingine walichosoma. Hali hii inadhihirika bayana katika jedwali lifuatalo;

Jedwali la 3. Asilimia za swali la Maudhui/Mafunzo

Swali la hojaji	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Kitabu hiki kimenipa mafunzo mengi na mazuri kuliko cha pili.	172x100 265 =64.91%	138x100 195 =70.76%	82x100 135 =60.74%

Hata ingawa wanafunzi walipata mafunzo mengi kutoka kitabu cha *Mtu wa Mvua*, ni dhahiri kwamba hakukuwa na tofauti kubwa ya miitikio katika vitabu vya *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni.*

4.3.2. Anwani ya Vitabu

Anwani ya *Ndoto ya Amerika* ndiyo iliyowapendeza watoto zaidi kuliko ile ya *Mtu wa Mvua* na *Mgomba Changaraweni.* Asilimia 74.55 ya wanafunzi waliosoma kitabu cha *Ndoto ya Amerika* walipendezwa na anwani ya kitabu hiki ikilinganishwa na anwani za vitabu vile vingine.

Jedwali la 4. Asilimia kuhusu swali la Anwani ya kitabu.

Swali la hojaji	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Niliipendwa anwani ya kitabu hiki kuliko kile cha pili.	$\frac{164}{265} \times 100$ = 61.88%	$\frac{114}{195} \times 100$ =58.46%	$\frac{70}{135} \times 100$ =51.85%

Hapa ilionekana kwamba watoto walipendezwa na anwani ambazo ziliwapa matumaini ya kuzuru nchi tofauti. Amerika ni nchi ambayo inasifika kwa mambo mengi ambayo yalifanya watoto wengi kutaka kujionea. Habari kuhusu nchi hii walizipata kutoka kwa walimu, marafiki, ndugu, vyombo vya habari na wazazi wao.

4.3.3 Majalada ya Vitabu

Asilimia kubwa ya miitikio ya watoto wasomaji ilidhihirisha kwamba jalada la kitabu cha *Mtu wa Mvua* ndilo lililokuwa bora zaidi kuliko majalada ya vitabu vya *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni.* Asilimia hii ilikuwa 67.18 kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo;

Jedwali la 5. Asilimia kuhusu swali la majalada ya vitabu

Swali la Utafiti	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Nililipenda jalada la kitabu hiki kuliko kile cha pili.	163x 100 265 =61.51%	131x100 195 =68.18%	69x100 135 =51.11%

Jalada huwa na picha, anwani na rangi iliyochaguliwa. Picha katika jalada la kitabu cha *Mtu wa Mvua* ilikuwa ya Mtu wa Mvua mwenyewe kama anwani ya kitabu ilivyoashiria. Vipengele hivi basi vilileta maswala ya uajabuajabu katika kitabu cha *Mtu wa Mvua* kuanzia mwanzoni. Uajabu ajabu ni kipengele walichopenda sana watoto maanake kiliwatoa katika ulimwengu halisi na kuwaingiza katika ulimwengu usio wa kawaida. Vilevile, kutokana na maoni niliyopata kutoka kwa watoto wa shule zote mbili, ni kwamba watoto hupendezwa na kitabu ambacho anwani yake na picha inayofuatia katika jalada inavutia na zote pamoja zinampa fununu ya yale anayotarajia kupata ndani ya kitabu. Rangi zilizotumiwa zilikuwa za samawati na nyekundu kiasi. Matumizi ya

rangi nyekundu ilinata makini ya watoto wasomaji kisha rangi ya samawati ilitumika mara nyingi kuashiria maji (mvua katika misingi hii iliashiriwa vyema kwa rangi ya samawati).

Anwani ya *Ndoto ya Amerika* kwa kiasi ilikuwa na utata wake maanake mtoto hakujua iwapo ni Amerika ilikuwa ikiota au ni mtoto aliyechorwa katika kitabu aliyekuwa akiota. Hata hivyo, asilimia ya miitiko katika swali hili ilikuwa zaidi ya 60 kuonyesha kwamba baadhi ya wasomaji wa kitabu cha *Ndoto ya Amerika* walipendezwa na jalada la kitabu hiki. Anwani ya *Mgomba Changaraweni* nayo ilikuwa ya kimafumbo na watoto hawakuielewa anwani hii mara ya kwanza walipopata kitabu kile. Aidha, mtoto pia hakuweza kulinganisha anwani ya *Mgomba Changaraweni* na picha ya msichana na mvulana zilizowekwa pale katika jalada.

4.3.4 Wahusika

Watoto wasomaji walifurahishwa na wahusika wa kitabu cha *Mtu wa Mvua* kuliko vitabu vile vingine viwili. Hali hii ilidhihirishwa na jedwali ndogo lifuatalo:

Jedwali la 6. Asilimia kuhusu swali la Wahusika.

Swali la hojaji	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Wahusika wa kitabu hiki walinipendeza zaidi na kuniburudisha kuliko wale wa kitabu cha pili.	147x 100 265 =55.47%	125x100 195 =64.10%	73x100 135 54.07%

Kitabu cha *Mtu w Mvua* kilikuwa na hadithi fupi tatu kikilinganishwa na vitabu vile vingine viwili ambavyo vilikuwa na hadithi moja tu. Kwa njia hii, kitabu cha *Mtu wa Mvua* kiliwapa watoto wasomaji wahusika wengi wakuu ambao watoto waliweza kujinasibisha nao. Kuwepo wahusika wengi katika kitabu cha *Mtu wa Mvua* kulipelekea kuzuka kwa miktadha mbalimbali ya maisha ambayo iliakisi maisha halisi ya watoto wasomaji. Hivyo basi, hali hii iliwapelekea watoto wasomaji kupenda wahusika wa kitabu cha *Mtu wa Mvua* kuliko vile vingine viwili. Mahojiano yangu na wanafunzi yalibainisha wazi kwamba watoto wengi walikuwa wakiwataja na kujinasibisha na wahusika wa kitabu cha *Mtu wa Mvua*. Baadhi ya wahusika waliotajwa pamoja na sifa zao walikuwa kama kama wafuatao: Dora aliwavutia kwa sababu umri wake ulikuwa mdogo, namna ambavyo aliajabia Okungu, maswali aliyokuwa akimuuliza Okungu na namna ambavyo alitumia mbinu ya wimbo kumsifu Okungu (uk 45). Okungu alivutia kwa sababu ya miujiza yake; fimbo iliyoweza kuwarudisha ng'ombe walioibwa nyumbani, kutonyeshewa akiwakamua ng'ombe, kuwafanya wezi kusalimisha bunduki walizokuwa nazo bila kuzua rabsha na namna ambavyo alikuwa akitembea katika mvua bila kunyeshewa. Mhusika Charo katika *Charo na Watoto Watoro* aliwavutia sana watoto wasomaji kutokana na utundu wake; Kuhusika kwake na watoto watoro kulileta picha halisi ya ulimwengu wa watoto kutaka kuvumbua mambo. Charo hapa alikuwa kielelezo cha uhalisi wa maisha yao. Udanganyifu wake ulizua burudani kwa watoto wasomaji. Katika hadithi *Sungura Hasara* ile hali ya mtoto kupewa jina la lakabu katika maisha halisi kutegemea tabia zake kuliwafurahisha sana watoto wasomaji. Nilipowauliza watoto wasomaji iwapo walikuwa na majina ya lakabu, walikubali kwamba ndugu zao, wazazi

wao na wengine katika jamii walikuwa wamewapa majina ya lakabu. Sungura Hasara aliitwa hivyo kwa kumuibia kakake picha kisha akadai shuleni kwamba ndiye aliyekuwa mchoraji.

4.3.5 Ugumu/wepesi wa hadithi.

Hadithi iliyokuwa nyepesi kueleweka kwa misingi ya mtoto msomaji ilikuwa *Ndoto ya Amerika* kama asilimia zilivyoonyesha katika jedwali lifuatalo:

Jedwali la 7. Asilimia kuhusu Ugumu/Wepesi wa hadithi.

Swali la utafiti	Ndoto ya Amerika	Mtu wa Mvua	Mgomba Changaraweni
Niliielewa hadithi ya kitabu hiki kwa urahisi kuliko kile cha pili.	172x100 265 =64.91%	120x100 195 =61.54%	74x100 135 54.81%

Ugumu /wepesi wa hadithi husabishwa pakubwa na ploti. Kiwango cha lugha vilevile ni kisababishi kikuu cha ugumu wa ploti. Katika fasihi ya watoto, ploti kwa mujibu wa Freitag (1972:20) ni za aina tatu:

(i) Ploti sahili

(ii) Ploti changamani

(iii) Ploti taharuki

Katika kitabu cha *Ndoto ya Amerika*, mwandishi Ken Walibora alifanikiwa kutumia aina moja ya ploti. Katika hatua za kwanza za hadithi, mwandishi alitutambulisha kwa

mhusika Isaya Yano ambaye alikuwa na hamu kubwa ya kwenda Amerika. Mvulana huyu (ambaye alilelewa mashambani) aliamua kufunga safari kwenda jijini ili kujiandaa kwenda Amerika. Kwa kusimulia utangulizi kama huu wa hadithi, mwandishi aliweka wazi mtiririko wa vitushi utakavyokuwa. Mtoto msomaji alitarajia kwamba mtiriko wa vitushi utakuwa wa moja kwa moja, hali ambayo ndiyo teneti kuu katika ploti ya moja kwa moja. Hii ndiyo aina kuu ya ploti aliyotumia mwandishi.

Kuanzia sura ya tatu ya hadithi, mwandishi alizua migogoro mbalimbali iliyomsaidia kuijenga ploti. 'Utamu' wa hadithi ulizidi pale mhusika Isa alikuwa na migogoro katika nafsi yake, kati yake na mazingira, kati yake na watoto wenzie, kisha kati yake na jamii kwa jumla. Madoa alimtuliza Isaya Yano kwa kumwambia kwamba asiwe na wasiwasi maanake yeye mwenyewe alijua namna ya kufika Marekani. Kisha baadaye Madoa alimwelekeza Isaya Yano kwa jambazi (Rock Mwamba) ambaye alikuwa mhalifu mkubwa jijini Nairobi. Katika hali hii, Isa ana imani kwamba atafika Marekani ila mambo yalikuwa kinyume baadaye alipojipata mahakamani kwa shtaka la kushirikiana na mhalifu sugu Zablon Okutoyi (Rock Mwamba) aliyekuwa akitafutwa na polisi kwa muda mrefu.

Mtiririko wa hadithi kama huu ulimwingiza mtoto moja kwa moja katika hali halisi ya maisha ya watoto wa umri wake. Kipindi cha umri wa miaka 12-16 hushuhudia watoto kuwa wakaidi kiasi kwa wazazi wao kama alivyokuwa Isaya Yano. Watoto walisema kwamba hiki ndicho kipindi cha wao kunaswa na kuathiriwa pakubwa na matendo ya watoto wenzao kama alivyonaswa Isa na kisha baadaye akaathiriwa na matendo ya Madoa. Ni kipindi ambacho watoto hupenda kufanyia utafiti yasiyowezekana vilevile. Mfano unadhihirika wazi katika ndoto aliyokuwa nayo Isaya Yano ya kwenda

Amerika: kwa uhalisia, safari ya kwenda Amerika ina utaratibu wake tofauti na utaratibu aliokuwa nao Isaya Yano.

Mtoto msomaji hakusumbuka katika kujaribu kuoanisha kitushi na kingine. Vitushi vilikuwa na mtiririko ulioeleweka na mtoto msomaji. Vitushi vilipokezana kwa utaratibu; hali ambayo ilimfanya mtoto afuatilie mtiririko wa hadithi pasipokuwa na usaidizi wowote. Hivyo basi, ilidhihirika bayana kwamba watoto wa umri 12-16 walihitaji hadithi ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa na ploti ya moja kwa moja.

Watoto walitaja kwamba ugumu wa hadithi katika *Mtu wa Mvua* na *Mgomba Changaraweni* ulisababishwa na ploti ya hadithi zenyewe, tamathali za lugha alizotumia mwandishi pamoja na maudhui aliyoshughulikia mwandishi. Kitabu *Mtu wa Mvua,* kilikuwa na hadithi nyingi: hali ambayo iliwafanya watoto wachanganyikiwe walipozisoma. Ploti za hadithi mbalimbali zilikuwa zikitofautiana katika kitabu cha *Mtu wa Mvua.* Ugumu wa *Mgomba Changaraweni* ulianzia katika anwani yenyewe maanake maana ya tamathali hii ya usemi aliyotumia Ken Walibora ilidhihirika bayana mwishoni mwa kitabu (kwa baaadhi ya wanafunzi tu) Wanafunzi wengine walisema kwamba hawakuweza kukisoma kitabu cha *Mgomba Changaraweni* hadi mwisho kutokana na ugumu wake.

4.3.6 Matumizi ya picha

Hapa, asilimia kubwa zaidi ya miitikio iliweka bayana kwamba picha katika kitabu *Mtu wa Mvua* zilikuwa za kupendeza zaidi kuliko vitabu vile vingine viwili; Hali hii ilidhihirishwa na jedwali ndogo lifuatalo:

Jedwali la 8. Asilimia kuhusu matumizi ya picha.

Swali la utafiti	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Picha katika kitabu hiki zilikuwa za kupendeza kuliko kile cha pili.	107x 100 265 =40.37%	149x100 195 =76.41%	64x100 135 =47.41%

Picha katika *Mtu wa Mvua* zilikuwa zimekolezwa rangi mbalimbali zikilinganishwa na picha katika kitabu *Ndoto ya Amerika* ambazo hazikuwekwa rangi kamwe. Katika hadithi ya *Mtu wa Mvua*, picha za Dora, Mtu wa Mvua, mamake, mazingira ya pale nyumbani pamoja na picha za wezi waliosalimisha bunduki zilikuwa za kupendeza kwa sababu zilikolezwa rangi. Katika hadithi ya *Sungura Hasara*, picha ya Sungura hasara mwenyewe akicheza 'lifundo' na mwenzake ilikuwa ya kuvutia kama walivyosema watoto. Picha zingine zilizovutia zilikuwa za Fumbo alipokuwa amesimamishwa na mwalimu mkuu mbele ya wanafunzi wenzake baada ya kulaghai kwamba angeweza kuchora picha ukutani (uk. 27) Katika hadithi ya *Charo na watoto watoro*, picha ya Charo na wenzake wakinusa gundi ilikuwa ya kupendeza hasa kwa wavulana waliosoma kitabu hicho. Kwa ujumla, mwandishi alitumia rangi ya buluu, kijani kibichi, nyekundu, majano na nyeusi katika kitabu *Mtu wa Mvua*. Hali hii ilidhihirisha kwamba watoto walipenda vitabu ambavyo maandishi yaliandamana na picha kisha picha zile zikolezwe rangi anuwai. Haya yalithibitika pia katika mahojiano

yangu na watoto wasomaji. Picha katika *Mgomba Changaraweni* zilikolezwa aina moja ya rangi tu: rangi ya kijani kibichi.

4.3.7 Lugha katika vitabu vyote vitatu.

Asilimia 68.21 ya wanafunzi waliochagua kitabu cha *Mtu wa Mvua* walisema kwamba lugha ya Kiswahili katika kitabu hiki ilikuwa nyepesi kueleweka. Katika mahojiano, walidai kwamba haikubidi watumie kamusi kwa wingi au kuuliza maana ya msamiati waliposoma kitabu cha *Mtu wa Mvua.*

Jedwali la 9. Asilimia kuhusu lugha katika vitabu vyote vitatu.

Swali la hojaji	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Lugha katika kitabu hiki ilikuwa nyepesi kueleweka kuliko kile cha pili.	139x100 265 =72.27%	123x100 195 =76%	71x100 135 =60%

Baadhi ya wale waliosoma kitabu cha *Mgomba Changaraweni* walidai kwamba kitabu hiki kilikuwa na baadhi ya maneno na miundo ya sentensi za Kiswahili ambazo zilikuwa ngumu kueleweka. Kiwango cha lugha killikuwa kipengele muhimu katika kuibua hisia za mtoto msomaji kuhusiana na kitabu alichokisoma. Watoto wasomaji walikielewa na kukipenda sana kitabu ambacho lugha iliyotumika ilikuwa rahisi kueleweka.

4.3.8 Umwafaka wa Kitabu

Kulingana na kamusi ya Kiswahili ya TUKI, maana ya mwafaka ni kitu kinachofaa au kinachostahili. Katika utafiti huu, tulitumia umwafaka wa kitabu kumaanisha kufaa au kustahili kwa kitabu kwa wasomaji walengwa. Kunavyo vigezo mbalimbali vya kupima umwafaka wa kitabu cha fasihi ya watoto. Katika utafiti huu, tulijikita katika vigezo ambavyo viliwathamini watoto kama wadau wakuu katika kupima umwafaka wa fasihi aliyoandikiwa. Kwa kujaza hojaji na kwa kuwahoji wanafunzi waliosoma kitabu cha *Mtu wa Mvua,* walidai kwamba kwa asilimia kubwa kitabu hicho ndicho kilikuwa mwafaka zaidi kwao kikilinganishwa na vingine walivyovisoma. Hali hii ilidhihirishwa na jedwali lifuatalo:

Jedwali la 10. Asilimia kuhusu umwafaka wa vitabu.

Swali la utafiti	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Kitabu hiki kinastahili kusomwa na wasomaji wa umri wangu	139x 100 265 =52.45%	123x100 195 =63.08%	71x100 135 52.59%

Licha kwamba watoto wengi walikichangamkia kitabu *Ndoto ya Amerika* katika hatua ya kwanza, ni watoto wachache waliodai kwamba kitabu hicho kilistahili kusomwa na watoto wa umri wao. Nilipowauliza maoni yao kuhusiana na kitabu *Mgomba Changaraweni,* baadhi yao walisema kwamba kilikuwa na maudhui ya kuwapotosha.

(yaani mapenzi) Nilipowauliza wanafunzi sababu za kuchagua *Mtu wa Mvua* walisema kwamba *Mtu wa Mvua* kilikuwa na mambo anuwai ambayo yaliakisi maisha ya kila siku.

Kwa ujumla, swali hili la umwafaka lilikuwa maoni ya kijumla ya mtoto mwenyewe kuhusiana na vitabu alivyovisoma. Nilipowahoji, sababu nyingi walizozitoa zilikuwa muhutasari wa sababu mojamoja walizotoa katika maswali ya mwanzo katika kitengo cha ujazaji wa hojaji pamoja na kitengo cha mahojiano.

4.3.9 Idadi ya hadithi katika kitabu.

Kitabu *Mtu wa Mvua* kilichokuwa na hadithi tatu ndani yake kilipendwa zaidi na watoto wasomaji kuliko vile vingine ambavyo vilikuwa na hadithi moja pekee. Hali hii ilidhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali la 11. Idadi ya hadithi katka kitabu.

Swali la utafiti	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
Nilikipenda kitabu hiki kwa sababu kilikuwa na hadithi moja pekee/zaidi ya moja.	137x 100 265 =51.70%	124x100 194 =63.59%	64x100 135 =47.41%

Katika hali hii, ilikuwa dhahiri kwamba watoto wasomaji walipenda kitabu ambacho kiliwapa hadithi zaidi ya moja kuliko kile ambacho kilikuwa na hadithi moja pekee.

Wanafunzi walivipenda vitabu vile vingine vilivyokuwa na hadithi moja kwa asilimia 51.70 na 47.41.

4.4 Hitimisho

Baada ya kutarakilisha miitikio kiasilimia kutegemea na maswali ya hojaji na madhumuni ya utafiti, wastani kiasilimia wa kila kitabu ulitafutwa ili kubainisha kitabu kilichokuwa mwafaka zaidi. Jedwali lililofuata lilionyesha bayana asilimia zilizopatikana:

Jedwali la 12. Wastani jumla wa miitikio kutokana na hojaji


Kitabu	*Ndoto ya Amerika*	*Mtu wa Mvua*	*Mgomba Changaraweni*
WASTANI KWA ASILIMIA (%)	57.02%	65.93%	51.85%

Kitabu cha *Mtu wa Mvua* kilikuwa mwafaka kwa misingi ya mbinu ya Likert niliyotumia. Asilimia ya miitikio iliyopatikana ilikuwa 65.93. Kilifuatia kitabu cha *Ndoto ya Amerika* ambacho asilimia ya miitikio yake ilikuwa 57.02. Mwisho kabisa kilikuwa kitabu cha *Mgomba Changaraweni* ambacho asilimia ya miitikio ilikuwa 51.85. Hali hii ilionyesha kwamba kunavyo vipengele mbalimbali katika vitabu viwili vya mwisho ambavyo viliathiri viwango vya umwafaka.

Asilimia hizi za wastani zilizopatikana ziliwekwa katika grafu kwapao kama ifuatavyo:

Grafu 1. Grafu kwapao ya umwafaka wa vitabu.

1. *Mtu wa Mvua* 65.93%
2. *Ndoto ya Amerika* 57.02%
3. *Mgomba Changaraweni* 51.85%



SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaanza kwa kutoa hitimisho. Hitimisho yenyewe ni muhutasari wa matokeo ya utafiti yanapolinganishwa na madhumuni yetu ya utafiti.

Pili nimetoa mapendekezo kuhusuana na maneno mapya ya kufanyiwa utafiti yaliyobainika wakati wa utafiti huu.

5.2 Hitimisho

Hatua zote tatu za ukusanyaji deta zilidhihirisha kwamba watoto wasomaji walikuwa na miitikio mbalimbali walipochagua kitabu miongoni mwa vitabu vitatu vya fasihi ya watoto vilivyoandikwa na Ken Walibora. Kwamba, watoto waliweza kuchagua vitabu viwili vilivyowaridhisha zaidi miongoni mwa vitatu vilivyowekwa mezani katika hatua ya kwanza. Baada ya kusoma vitabu viwili walivyovichagua, walikuwa na uwezo wa kutambua kitabu kilichokuwa mwafaka zaidi kwao.

Uchanganuzi wa hojaji uliweka wazi kwamba kitabu cha *Mtu wa Mvua* ndicho ambacho kilikuwa mwafaka zaidi kwa watoto wasomaji. Kwa misingi ya miitikio iyohiyo, kitabu cha *Ndoto ya Amerika* kikachukua nafasi ya pili huku kile cha *Mgomba Changaraweni* kikichukua nafasi ya tatu.

Kwa misingi ya miitiko iliyopatikana basi, ilibainika wazi kwamba watoto wanao uwezo wa kujiteulia kitabu mwafaka miongoni mwa vitabu kadhaa vya mwandishi wa fasihi ya watoto. Katika utafiti wetu, watoto wasomaji walijiteulia kitabu cha *Mtu wa*

Mvua kama kitabu mwafaka zaidi miongoni mwa vitabu vitatu vya Ken Walibora vilivyoshirikishwa katika utafiti.

Ni muhimu nitaje kwamba matokeo haya ni tofauti na hali iliyopo sasa kuhusiana na vitabu vya fasihi ya watoto vya Ken Walibora. Shirika la uchapishaji la Sasa Sema lilikitukuza kitabu cha *Ndoto ya Amerika* kuwa ndicho kilikuwa kitabu mwafaka zaidi kwa watoto wasomaji. (Rejelea tangazo kwenye jalada la kitabu *Ndoto ya Amerika* pamoja na kwenye mtandao http:www.walibora ken/ndoto ya amerika/). Haijulikani walitumia vigezo gani ili kuibuka na maoni hayo. Labda inawezekana kwamba walitegemea wahakiki waliokomaa kuzuka na maoni haya. Katika utafiti huu watoto (ambao ndio hadhira lengwa ya vitabu vyote vitatu alivyowaandikia watoto) walikana kauli hiyo na kupendekeza *Mtu wa Mvua* kuwa bora zaidi kuliko *Ndoto ya Amerika.* Kwa kurejelea hali iliyopo sasa, (kwamba *Ndoto ya Amerika* ndicho kitabu mwafaka zaidi) basi ipo haja ya kufanyia ulinganishi wa miitikio ya watoto na ile ya watu wazima katika tafiti za siku za usoni.

5.3 Mapendekezo

Kuna haja ya kufanyia utafiti miitikio ya watu wazima wanaposoma fasihi ya watoto na kuilinganisha na miitikio ya watoto wanaposoma vitabu hivyo pia. Hali iliyopo sasa ni kwamba kitabu cha *Ndoto ya Amerika* kinapigiwa debe sana kama chapisho mwafaka la Ken Walibora. Hili wamekana watoto katika utafiti na kusema kwamba kitabu mwafaka zaidi ni *Mtu wa Mvua.* Hakujawa na utafiti unaolinganisha miitikio kutoka pande hizi mbili. Utafiti kama huu utaweka wazi iwapo watu wazima na watoto wanayo miitikio inayolingana. Matokeo ya utafiti kama huu yatasuluhisha malumbano

ambayo yamekuwepo kuhusu nani hasa anastahili kumchagulia mtoto vitabu vya fasihi ya watoto (Mwanzi, 1982)

Swala la wahusika vilevile lilizua eneo mufti la utafiti. Baadhi ya wasichana walijaribu kujinasibisha na wahusika wa kike licha kwamba hawakuwa wahusika wakuu katika vitabu hivi vitatu. Wavulana kwa upande wao walijihusisha na wahusika wa kiume hata ingawa wengi wao walikuwa wahusika wakuu. Katika swala hili, palitokeza maeneo mawili ya utafiti; eneo la kwanza ni kuchunguza wahusika wakuu wa vitabu vya watoto ni wa jinsia gani. Na pili, ni kuchunguza namna ambavyo watoto wasomaji hujinasibisha na wahusika katika vitabu kutegemea jinsia yao.

MAREJELEO.

Akoleit, J. (1990) *Response and Critisicm in Children's Literature in Kenya. The case of Barbara Kimenye.* Unpublished M.A. Thesis Kenyatta University.

Alembi, E..(1992) *An analysis of the style and social significance of the Abanyole Children's Oral poetry.* M.A. Thesis Kenyatta University.

Alcott's (1868) *Little Women.* Bantan Books Publishers England

Ashliman, D. (2006) *The Grimm Brothers'Children's and Household Tales (Grimms' Fairy Tales)* Grimm J. by Grimm W. 1885).

Ashliman, *D.* (2006) *The Tales of Mother Goose by Charles Perrault* - Project Gutenberg

Atwood, J. (1982) *Second Words*:Toronto. House of Anansi Press.

Benton, M. et. al.(1985) *Teaching Literature 9-14* .Oxford. Oxfod university Press.

Bylan, E. (1991) *Women and Disability.* Zed books Ltd. London and New Jersey.

Brumfit C.J. et. al.(1986) *Literature and Language* Teaching. Oxfford university press

Carrol, L. (1865) *Alice's adventure in Wonderland* Dodgson math Proof Oxford

Cass, J. (1984) *Literature and the Young Child.* Heinman Publishers London.

Comenius (1568) *Latin Through Pictures* (Orbis Sensulium pictus 1568. published in Nuremberg

Coody, B. (1973) *Using Literature with Children*. Brown Company Publishers U.K.

Emenyonu, E.N.(1990) *Literature and Black Aesthetics*: Heinman Educational books (Nigeria) Ltd.

Fish, S. (1980) Is *There a Text in This Class? The Authority of Interpretive Communities*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.

Friends, S. (1993) New Introductory Lecture on Psychoanalysis. Translated and edited by James Stachey. Newyork Norton.

Fry, E.(1968) *A Readability Formula that Saves time*. Journal of Reading No. 11.

Gilliland, J. (1972) *Readability* London Hodder and Stough Publishers.

Graham, H.(1966) *An Essay on Critisicm* Pubblished by Gerald Ducksworth and Co. Ltd London.

Gross, R. (1963) *The Teacher and the Tought*. Newyork Dell Publishing Co. London.

Harthorn, J. (1987) Unlocking the Text. *Fundamental issues in Literary theory*. London. Edward Anold.

Hunt, Peter (1996). *International Companion Encyclopedia of Children's Literature*. London: Routledge

Hunt, P.(1994) *An Introduction to Children Literature*. Oxford University Press.

Hunt, P. (1992) *Literature for Children. Contemporary Criticism.* Routledge publishers. Newyork

Hunt, P. (1991) *Criticism Theory and Children Literature*, Oxford: Blackwell

Hunt, P. (1982) *Children's Literature Research in Britain Cardiff.* University of Wales Institute of Technology

Kimenye, B. (1967) *Moses and Mildred.* Nairobi: Oxford University Press, 1967.

Kitonga, E.(1984) *Children Literature in Kenya* .Presented in the IFLA 50th general Conference held in Nairobi.

Kiai, G.(1994) *Literature and Ideology in Children's Literature*. Paper presented at 3rd Pan- African book Fair in Nairobi.

Kibadi, I.M (1992) *A study of the Availability and Relevance of Children's Recreational Literature in selected public Libraries in Kenya.* Unpublished M.ed.Thesis Kenyatta University.

Kimble, G.A.et.al. (1980) *Principles of general Psychology.* Johwiley & Sons, Inc. U.S.A. 5TH Edition

Lesnik-Oberstein, Karin (1994) *Children's Literature: Criticism and the Fictional Child.* Oxford: Clarendon Press

Mabel, S. (1988) The Importance of Illustrations in Children's Books. Illustrations for Children. *A pulication of children literature Association of Nigeria.*

Maillu, D.G. (1997) *Atendaye Mema.* Jommo Kenyatta Foundations.

McGillis, R. (1985) The Child as a Critic.Using Children's Responses in the University Classroom. *Children's Literature Association Quarterly. 10(1)*

Michelle, L.(1993) *Children in Crisis.* Scholastic Canada Ltd.

Mwanzi, H.O.A.(1998) *Children's Literature in Kenya.*Unpublished M.A Thesis,University of Nairobi.

Newbery, J.(1744) *Little Pretty Ocket Book.* Published in London, England.

Nyambura, M..A. (1979) *Kikuyu Oral Literature and change with special reference to the Tale.* Unpublished M.A Thesis University of Dar-es-Salaam.

Nyambura, M.A. (1995) *Children's Literature in Tanzania:A literary appreciation of its growth and development.* M.A Thesis. Kenyatta University.

Odaga, A.B. (1985) *Literature for Young People in Kenya.* Makala iliyowasilishwa katika kongamano la fasihi. Nairobi.

Phoebe, A.M.(1992) *Publishing for children in Kenya.* Dissertation submitted to Oxford University.

Rosenblatt, L. M. (1985) Literature As Exploration: *Modern Language Association.* 5th ed. New York.

Rosenblatt, L. M.(1978) *The Reader, the Text, the Poem.* Carbondale, IL: Southern Illinois University Press.

Sampson, G.(1971) *Reader-Responses to Literature.* Routledge Publishers. U.K.

Stevenson, R.(1863) *Treasure Island.* Bantam Books Publishers England

Swift J. (1906) Gulliver's Travels and Other Works Routledge, 1906

Urquhart, F. (1907) "Foxe's Book of Martyrs" in *The Catholic Encyclopedia, Volume II* Copyright © 1907 by Robert Appleton Company

Walibora, K. (2001) *Ndoto ya Amerika.* Sasa sema publications Ltd. Nairobi

Walibora, K. (2004) *Mtu wa Mvua.* Phoenix publishers Ltd. Nairobi

Walibora, K. (2003) *Mgomba Changaraweni.* Phoenix publishers Ltd. Nairobi.

Wamitilla, K. (2002) *Uhakiki wa fasihi. Misingi na vipengele vyake.* Phoenix Publishers Ltd.

MAREJELEO KUTOKA KWENYE MTANDAO.

http://dictionary.cambridge.org/ 06/09/2007. 11.30A.M

http://www.ala.org/ala/alsc/awardsscholarships/literaryawds/literaryrelated.htm

2007 Literary and Related Award Winners 06/09/ 2007. 2.00PM

http://history.hanover.edu/courses/excerpts/165rouss-em.html Emile (1762)

15/10/2007. 9.00PM

http://www.gutenberg.org/etext/17208. 15/10/2007. 11.00PM

http://www.pitt.edu/~dash/grimmtales.html. 21/11/2007. 9.00A.M.

http://dictionary.reference.com/ 13/09/2007 12.30P.M.

http://www.yourdictionary.com/ 14/09/2007 9.30A.M.

http://en.wikipedia.org/wiki/Sampling(statistics) 17/09/2007 3.00 P.M.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A

Hojaji kwa mwanafunzi

SEHEMU A: Barua –tangulizi kwa mwanafunzi.

Kwa mwanafunzi mpendwa,

Kunao utafiti unafanywa kuhusu mwitikio wa mwanafunzi kwa vitabu vya fasihi. Mtafiti amekuteua wewe binafsi kama mshiriki katika utafiti huu na majibu yako yatakuwa muhimu kuufanikisha. Tafadhali unaulizwa kutoa majibu yako kwa uaminifu. Majibu utakayotoa yatahifadhiwa kwa usiri mkubwa.

SEHEMU B: Deta ya kibinafsi.Weka alama (✕) palipo na alama ( )

Shule:.....Umri.....

Jinsia: Mvulana Msichana

Darasa: La7 La 8

SEHEMU C: Tafadhali onyesha msimamo wako kuhusu kauli zifuatazo kwa kuweka alama (✕) kwa jibu lako.

Kumbuka: <u>Jibu maswali ya vitabu viwili tu ulivyovichagua.</u>

Maana ya ufupisho;

N.S. –Nakubaliana Sana

N. – Nakubaliana

S.U. –Sina Uhakika.

S. – Sikubaliani

S.K. – Sikubaliani Kabisa.

Mtu wa Mvua

1.Kitabu hiki kimenipa mafunzo mengi na mazuri kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

2.Niliipenda anwani ya kitabu hiki kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

3. Nililipenda jalada la kitabu hiki kuliko lile la kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

4.Wahusika wa kitabu hiki walinipendeza zaidi na kuniburudisha kuliko wale wa kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

5.Niliielewa hadithi ya kitabu hiki kwa urahisi kuliko ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

6.Picha katika kitabu hiki zilikuwa za kupendeza kuliko kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

7.Lugha ya Kiswahili katika kitabu hiki ilikuwa nyepesi kueleweka kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

8.Kitabu hiki kinastahili kusomwa na wasomaji wa umri wangu.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

9.Maandishi ya kitabu hiki yalisomeka kwa urahisi kuliko yale ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

10. Nilikipenda kitabu hiki kwa sababu kilikuwa na hadithi zaidi ya moja.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

Mgomba Changaraweni

1.Kitabu hiki kimenipa mafunzo mengi na mazuri kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

2.Niliipenda anwani ya kitabu hiki kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

3. Nililipenda jalada la kitabu hiki kuliko lile la kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

4.Wahusika wa kitabu hiki walinipendeza zaidi na kuniburudisha kuliko wale wa kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

5.Niliielewa hadithi ya kitabu hiki kwa urahisi kuliko ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

6.Picha katika kitabu hiki zilikuwa za kupendeza kuliko kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

7.Lugha ya Kiswahili katika kitabu hiki ilikuwa nyepesi kueleweka kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

8.Kitabu hiki kinastahili kusomwa na wasomaji wa umri wangu.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

9.Maandishi ya kitabu hiki yalisomeka kwa urahisi kuliko yale ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

10. Nilikipenda kitabu hiki kwa sababu kilikuwa na hadithi moja pekee.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

Ndoto ya Amerika.

1.Kitabu hiki kimenipa mafunzo mengi na mazuri kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

2.Niliipenda anwani ya kitabu hiki kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

3. Nililipenda jalada la kitabu hiki kuliko lile la kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

4.Wahusika wa kitabu hiki walinipendeza zaidi na kuniburudisha kuliko wale wa kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

5.Niliielewa hadithi ya kitabu hiki kwa urahisi kuliko ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

6.Picha katika kitabu hiki zilikuwa za kupendeza kuliko kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

7.Lugha ya Kiswahili katika kitabu hiki ilikuwa nyepesi kueleweka kuliko kile cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

8.Kitabu hiki kinastahili kusomwa na wasomaji wa umri wangu.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

9.Maandishi ya kitabu hiki yalisomeka kwa urahisi kuliko yale ya kitabu cha pili.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

10. Nilikipenda kitabu hiki kwa sababu kilikuwa na hadithi moja pekee.

NS ( ) N ( ) S.U ( ) S ( ) SK ( )

KIAMBATISHO B.

Maswali yatakayoongoza mahojiano kati ya mtafiti na mtafitiwa.

1. Ni hadithi gani iliyokupendeza kati ya zile mbili ulizosoma?
2. Kwa nini hadithi hii ilikupendeza?
3. Taja wahusika waliokupendeza katika hadithi ulizosoma?
4. Walifanya nini cha kukupendeza?
5. Ni hadithi gani ilikupa mafunzo?
6. Taja mafunzo uliyoyapata?
7. Ni hadithi gani utamshauri mwenzako aisome?
8. Kwa nini utamshauri kuisoma?
9. Taja mhusika ambaye ungependa kuwa kama yeye?
10. Ni hadithi gani ilikuwa gumu kuelewa? Kwa nini?
11. Je uligundua makosa yoyote ya Kiswahili katika hadithi ulizosoma? Taja kosa/makosa ye/lenyewe?
12. Je ukitumwa dukani ukanunue kitabu kimoja miongoni mwa hivi vitatu utanunua kipi?

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY